# Nipashe

Ijumaa Julai 10, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580280

The Guardian digital

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN

The Global Religions for Children Foundation




## Hausiboi auawa akidaiwa kuua watoto wa bosi wake

UKURASA 7

# Wabunge CCM mbaroni kwa tuhuma za rushwa

**MMOJA** akutwa na fedha mfukoni akidaiwa kuhonga wajumbe, mwingine ang'ang'aniwa na TAKUKURU, makada 11 wasimamishwa uanachama ...*Endelea ukurasa 2, 3 na 7*




## Kitendawili mgombea wa urais CCM Zanzibar kuteguliwa leo

UKURASA 2

## NIA URAIS YASHIKA KASI ADC, CHADEMA

UKURASA 5


BAA LA CORONA



'USICHUKULIE POA UNATEGEMEWA'

- Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka
- Kaa kwa kuachiana nafasi hatua 2 au 3
- Vaa barakoa
- Ukikohoa au kupiga chafya ziba mdomo



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO SVEN ATENGA SAA 48 HATARI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. John Magufuli, akiimba wimbo wa chama pamoja na wajumbe wa Kamati Kuu, kabla ya kuanza kwa kikao hicho jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Kitendawili mgombea wa urais CCM Zanzibar kuteguliwa leo

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa (NEC), inatarajia kufanya kikao chake leo jijini Dodoma, kuchagua jina moja la mwanachama atakayesimama katika uchaguzi wa urais wa Zanzibar.

Katika mchakato wa kuchukua fomu ya urais huo, walijitokeza wagombea 33 ambapo Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa Zanzibar ilichuja na kupendekeza majina matano kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM (CC).

Hatua hiyo ya NEC itatokana na mapendekezo ya CC ambayo iliketi jana kupitia majina hayo matano.

Kwa mujibu wa kanuni za uteuzi wa wagombea uongozi katika vyombo vya dola toleo la Juni 2019, baada ya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa Zanzibar kuwachuja watia nia, majina matano yatapendekezwa kwa CC bila ya kupigiwa kura.

Kanuni hizo zinabainisha kuwa, CC itapitia sifa za wagombea hao na kupendekeza majina yasiyozidi matatu kwa NEC kwa ajili ya uteuzi wa mwisho.

Pia, NEC itapiga kura za siri kuchagua jina moja la mwanachama wa CCM atakayesimama katika uchaguzi huo kwa tiketi ya chama hicho, isipokuwa kwamba endapo Kamati Kuu itapendekeza jina moja tu, NEC itapiga kura za ndiyo au hapana.

Akizungumzia maandalizi ya vikao hivyo, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, alisema yanakwenda vizuri na wajumbe wameanza kufika kuanzia jana.

"Mkutano utakuwa na wajumbe zaidi ya 1,800 na wageni zaidi ya 1,000, mkutano wetu mkuu wa taifa utaketi Julai 11 hadi 12 mwaka huu na maandalizi yote yamefanyika," alisema.

Alisema mkutano huo utatanguliwa na kikao cha CC na NEC ambavyo vitachagua mwanachama mmoja wa CCM atakayesimama kwa nafasi ya mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia kumtambulisha na kumwidhinisha mgombea mwenza na mgombea wa urais wa Zanzibar.

**KAULI ZA WACHAMBUZI**

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa kwa nyakati tofauti jana, waliiambia Nipashe kuwa ongezeko la wagombea wanaoomba ridhaa ya CCM kupeperusha bendera ya chama hicho Zanzibar, ni ishara kuwa nafasi ya urais sasa imezoeleka na kuona kila mtu anaweza kugombea.

Vilevile, walisema uamuzi wa kuficha majina ya wateule watano yaliyotoka Zanzibar kwenda Dodoma, ni ishara kwamba kuna hofu ya mganganyiko na makundi ya wagombea wa nafasi husika.

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa Mohammed Bakari, alisema uamuzi wa kutoweka wazi majina hayo umeondoa siasa za mgawanyiko na makundi.

Alisema kuwa kwa upande mwingine, wapo waliokuwa na haki ya kujua majina matano kabla hayajapelekwa Dodoma ili kuondoa minong'ono iliyopo kwa sasa, lakini wamekosa haki hiyo.

Wakili wa Mahakama Kuu Zanzibar, Awadhi Ali Saidi, alisema kujitokeza kwa watu wengi ni ujumbe kwamba urais wa nchi sasa unaonekana ni kitu cha kawaida na hakuna uzito wa majukumu tena, ilhali wadhifa huo unabeba majukumu mazito ya kuhakikisha maendeleo ya watu na uamuzi wa nchi.

"Tunachoona sasa watu wanaona urais ni raha tu, kama una nguvu ya elimu na cheo, basi wewe unaweza. Lakini hajui kuwa unabeba majukumu makubwa ya kiuongozi na unatakiwa kuwa na maono makubwa ya kuongoza nchi," alisema.

"Inaonekana kama mzaha mzaha tu kwamba kwa sababu mtu ana fedha, anachukua fomu, tulitarajia watu wauogope, ila sasa wanaona ni fursa ya kutangaza dhamira yao, wanachukulia kama jambo jepesi la mzaha mzaha."

Kuhusu watoto wa marais wastaafu kujitokeza katika kinyang'anyiro hicho, wakili huyo alisema hakuna katazo la kisheria wala kikatiba, lakini kisiasa inaleta picha isiyo nzuri ya uongozi wa kurithishana.

Saidi ambaye amewahi kuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Zanzibar, alisema kuwa siasa za Zanzibar hazitoi picha nzuri na suala hilo linapaswa kuangaliwa kwa jicho la pekee.

Alisema siasa za Zanzibar zinabadilika kulingana na mahitaji ya wakati na uongozi uliopo kwa wakati huo.

Kuhusu majina yaliyopendekezwa na CC, Polepole alisema taarifa hazitakuwa wazi na kuwataka watu wagombea waendelee kuwa wanyenyekevu na watulivu.

"Ukifanya mchezo tu kesho (leo) tunafanya utaratibu mwingine, kwa hiyo kesho (leo) kwenye NEC tutawaambia wajumbe ni kina nani Kamati Kuu imewapeleka NEC, wana-CCM tuendelee kuwa watulivu," alisema.

## Wabunge CCM mbaroni kwa tuhuma za rushwa

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

WABUNGE wawili kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliomaliza muda wao, wamekamatwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma kwa tuhuma za kutoa hongo kwa watu wanaosadikiwa kuwa wajumbe wa chama hicho.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa jana, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, aliwataja wawili hao kuwa ni aliyekuwa Mbunge wa Mtera, Livingstone Lusinde, na aliyekuwa Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Peter Serukamba.

Kibwengo, akifafanua kuhusu tuhuma dhidi ya Lusinde, alisema TAKUKURU ilipata taarifa Julai 7 mwaka huu kwamba alikuwa amewakusanya wajumbe wa CCM nyumbani kwake Mvumi wilayani Chamwino mkoani hapa, kwa ajili ya kuwahonga na kufanya ushawishi fulani.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa hiyo, maofisa wa taasisi hiyo walifika katika nyumba hiyo na kukuta watu wanaosadikiwa kuwa ni wajumbe wa CCM takribani 20.

"Wajumbe hao walikutwa nyumbani kwa mtuhumiwa, hatukukuta wakigawana fedha kama taarifa zilivyoeleza, isipokuwa walikuwa wameandaliwa chakula na walipoulizwa, walisema walikwenda huko kumwona mtu ambaye amejifungua.

"Lakini, kama tunavyojua, ukienda kumsalimia aliyejifungua, huwezi kwenda bila zawadi, hao wote hawakwenda na chochote," alisema.

Alisema kuwa baada ya kutilia shaka maelezo yao, maofisa hao walimkamata Lusinde na kuwekwa chini ya ulinzi na kusitisha mkutano wake na wajumbe hao.

"Suala lake lina picha mbili; kwanza wamsaidie yeye mtia nia na jingine wamsaidie Halima Okash ambaye ni mtia nia ya kugombea ubunge wa viti maalum. Kwa hiyo, yote tunaendelea na uchunguzi kuthibitisha hizi taarifa, lakini kwa sasa Lusinde ameachiwa.

"Lusinde alihojiwa jana (juzi), lakini atahojiwa tena leo (jana) au kesho (leo) kadri uchunguzi unavyoendelea. Pia, tunaye huyo Halima Okash, tunaendelea naye kwa mahojiano," alisema.

Kuhusu tuhuma dhidi ya Serukamba, kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema wanamshikilia kwa tuhuma zinazofanana na za Lusinde, ikidaiwa kuwa naye alikuwa akigawa rushwa zinazohusiana na Uchaguzi Mkuu kwenye Hoteli ya Dodoma.

Kibwengo alisema wanaendelea na msako wa watia nia wote wanaotegemea rushwa kushawishi kupitishwa kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi huo.

***HABARI ZAIDI UKURASA WA 3 NA 7**

HABARI KITAIFA

# Mbunge matatani madai ya rushwa

Na Joctan Ngelly, KIGOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kigoma imemkamata aliyekuwa Mbunge wa Buhigwe, Albert Ntabaliba, maarufu kama Obama (pichani), kwa tuhuma za rushwa.

Sambamba na Obama, kiongozi mwingine aliyekamatwa ni Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Buhigwe, Everina Muhungo. Wawili hao wanadaiwa kugawa fedha kwa wajumbe waliohudhuria kikao cha ndani kilichofanyika Julai 7, mwaka huu, katika Kata ya Mnanila wilayani humo.

Maofisa wa Takukuru waliokuchua fedha hizo zinazokadiriwa kuwa zaidi ya Sh. milioni 2.2 zilizokuwa zimepangwa kugawagawia wajumbe katika kikao hicho.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Kigoma, Stephen Mafipa, alisema Julai 6, mwaka huu, walipokea simu kutoka kwa wasiri wao kuwa Obama alikuwa akifanya vikao vya ndani kuelezea utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwenye kata mbalimbali wilayani humo.

Mafipa alisema vikao hivyo vilikuwa vikiambatana na utoaji wa fedha kwa wajumbe ambao alikuwa akikutana nao na kwamba kiwango cha fedha ambacho kilikuwa kikitolewa ni kulingana na idadi ya wajumbe.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, walifanya ufuatiliaji kwa kuwasiliana na CCM Wilaya na kuelezwa kuwa vikao anavyovifanya ni halali lakini kama kuna kitu kingine kinatokana na vikao hivyo ambacho ni vitu vya thamani si halali.

Baada ya hapo, alisema Julai 7 aliwatuma maofisa wake kwenda Buhigwe kufuatilia vikao anavyovifanya ambavyo kwa mujibu wa taarifa vilikuwa vimalizike jana.

Kwa mujibu wa Mafipa, maofisa wa TAKUKURU baada ya kwenda kufatilia vikao hivyo, walipenya na kuingia katika kikao ambacho kilikuwa kikifanyika katika Kata ya Mnanila majira ya saa 8:00 mchana.

Alisema baada ya kikao kumalizika, Muhungo alionekana akigawa fedha Sh. 10,000 kwa kila mjumbe na wakati huo anakamatwa alikuwa ameshagawa Sh. 210,000 kwa wajumbe.

Wakati anagawa fedha hizo, Mafipa alisema maofisa wa TAKUKURU waliingilia kati na kuzuia shughuli hiyo na kuamuru wajumbe wote ambao walikuwa wameshapokea fedha hizo, warudishe na Sh. 210,000 zilisalimishwa mbele ya maofisa wa TAKUKURU waliokuwapo kwenye kikao hicho.

Pia alisema maofisa wa TAKUKURU walimtaka Obama kusalimisha fedha zote alizokuwa nazo eneo hilo la kikao na kukabidhi Sh. Milioni mbili alizokuwa nazo.

Mafipa alisema fedha zote ziko katika ofisi za TAKUKURU mkoa wa Kigoma na upelelezi wa tukio hilo unaendelea na baada kumalizika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Pamoja na kukamata fedha hizo na kumtia mbaroni, Mafipa alisema taasisi yake ilimruhusu Obama kuendelea na vikao vyake kwa mujibu wa ratiba huku akitahadharishwa kutoendelea kugawa fedha.

Hata hivyo, Mafipa alisema baada ya kukamatwa, watuhumiwa hao walidai kuwa kikao kilitakiwa kianze majira ya saa 3:00 asubuhi, ndiyo maana aliwagawia fedha wajumbe hao kwa ajili ya chai.

Alisema baada ya kuchukuliwa maelezo ya awali, Muhungo alikiri kuwa Obama ndiye aliyempatia fedha hizo ili awagawie wajumbe baada ya kikao kumalizika.






RIPOTI MAALUM- 4

# Jumuiya Burunge hifadhi inayojiendesha kwa mtindo wa serikali, bajeti mabilioni

## ■Ijue inakoelekea na 'figisu' zake

**Na Salome Kitomari, aliyekuwa** BABATI

**JANA katika sehemu ya tatu ya mfululizo wa taarifa zinazohusu Jumuiya ya Hifadhi za Jamii (WMA) Burunge, kulikuwa na ufafanuzi wa kina unaohusu ilivyoasisiwa, nyendo zake kiuchumi na namna ilivyoguswa na pigo la corona kama ilivyo kwenye maeneo mengine ya kiuchumi na kijamii nchini. Endelea kufaidika na mengine yanayokihusu chombo hicho:**



Katibu wa Jumuiya ya Hifadhi ya Jamii ya Burunge, Benson Maise (katikati), akifafanua jambo kwa mwandishi wa habari, Salome Kitomari. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Emmanuela William. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MENEJA Msaidizi wa Hoteli ya Burunge Tinted, Jackline Macha, anataja sababu za kuwekeza kwenye eneo hilo ni mvuto lilionao kitalii, mandhari yanatoa ushuhuda wa moja kwa moja kwa wanyama wanapokuwa katika nyendo zao, eneo jirani na hoteli, pia Ziwa Burunge.

Anasema katika hoteli yenye jumla ya vyumba 38, huwa wanapokea wageni kutoka mataifa mbalimbali, akinyambua takwimu zao kwamba katika msimu usio wa utalii, huwa ni wastani wa wageni 30 hadi 50 hotelini na msimu wa utalii hupokea wastani wa wageni 120.

Kwa mujibu wa Macha, mbali na wageni wanaofikia hotelini, wengine huishi kwenye mahema ndani ya mandhari ya kitalii, mfumo unaotumiwa pia kupendwa sana na watalii katika sehemu nyingi.

Macha aliiambia Nipashe hivi karibuni kuwa, mpango mkakati wao wa kimasoko ulitikiswa na mlipuko wa maradhi ya corona, kwa mpango wao kuwapokea kundi la wageni tangu Aprili iliyopita, lakini wakaangukia mbadala wa kufunga hoteli kwa muda, hatua iliyoenda sambamba na wafanyakazi 40 kupewa likizo.

Katika mazungumzo yake na Nipashe, wakati taifa likiwa kwenye mlipuko wa corona, Macha alifafanua: "Kwa sasa (wakati huo) tumebaki (wafanyakazi) saba kwa ajili ya usafi, ni kutokana na hali ya biashara. Tunatarajia kupokea wageni wengi Julai mwishoni na wafanyakazi wote watarudishwa kazini."

Pia, katika kuhami mazingira ya hifadhi yawe rafiki kwa wanyama ambao ndiyo mvuto wa utalii, meneja huyo anasema wanashirikiana kulinda mazingira ikiwamo kuondoa mifugo inayoingia hifadhini kwa kuwa uzoefu wao unaonyesha wanyama hupakimbia mahali walipo wakiwaona binadamu.

**MAUAJI KWENYE USHOROBA**

Kimsingi, unapotaja ushoroba, maana yake halisi ni mapito ya wanyama kutoka eneo moja kwenda lingine. Hiyo kiasilia hutumiwa na wanyama ama kuzaliana au kutafuta madini maalum ya miili yao.

Katika eneo hilo kuna Hifadhi za Taifa Ziwa Manyara na Tarangire, zinazounganisha eneo hilo linaloendelea hadi kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Hifadhi za Serengeti na Masai Mara, iliyoko katika nchi jirani ya Kenya.

Benson Maise, Katibu wa Jumuiya hiyo, anafafanua kuwa, matumizi ya shoroba yametambuliwa na eneo hilo ndani ya WMA linalindwa kwa ushirikiano na vijiji wadau, kwa utaratibu wa watuhumiwa waharibifu kupelekwa vijijini kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zao ndogo.

Hata hivyo, Maise anakiri kuwapo kwa vikwazo kutoka barabara kuu ya Arusha-Babati, inayokatiza eneo hilo, akirejea utafiti unaoonyesha kuwapo kwa idadi kubwa ya wanyama wanaouawa kwa kugongwa na magari.

Anafafanua wanavyokusanya takwimu kwa kutumia pikipiki maalum, taarifa zikionyesha kila siku wanyama wanakufa. Anaendelea: "Wanyama wanauawa hasa katika eneo la ushoroba kuanzia Makuyuni hadi Kibao cha Tembo. Wengine wanagongwa wakubwa kama twiga."

Wakati Maise akishauri Wakala wa Barabara (TANROADS) kuweka alama kwenye eneo hilo tajwa, Mtafiti wa Wanyamapori wa Mradi wa Simba, Dk. Benard Kissui, anasema kipindi kati ya Januari na Desemba mwaka jana, wanyamapori 380 walikufa kwa kugongwa na magari katika eneo hilo la ushoroba.

**MIKASA YA UJANGILI**

Dk. Kissui anasema kuwa hadi kufikia nusu ya kwanza ya mwaka huu, kulikuwa na watuhumiwa 28 wa ujangili na kati yao, 27 walihukumiwa. Pia, kulikuwapo kesi mbili zilizofutwa na tisa zinaendelea kusikilizwa.

Maise anafafanua kuhusu vikwazo wanavyokumbana navyo katika udhibiti wa ujangili unaofanywa kwa lengo la kuua wanyama kwa ajili ya kitoweo, kuwa ni nyendo za watu na tabia zao.

Anafafanua namna wanavyokabili tatizo hilo, akitamka: "Tunashirikisha jamii ipasavyo kuhakikisha wanaelewa na imefika mahali wananchi wanaelewa wanyama ni mali yao na wanawalinda na kutoa taarifa."

Katibu huyo anatoa simulizi ya mfano wa mkasa wa ujangili uliowatokea Aprili 21 mwaka huu, watu wasiojulikana walipowapeleka pundamilia 11 na mtoto wa twiga hadi liliko Ziwa Manyara na kisha wakawachoma mikuki.

"Pundamilia huwa haingii kwenye maji. Walichofanya, waliwalazimisha kuingia na wakawachoma wakafa. Tulifanikiwa kuchukua mabaki ambayo tunatarajia kutengeneza sehemu ya kumbukumbu, ili itumike kutoa elimu kwa vizazi," anasema Maise, akifafanua walikamatwa watuhumiwa 17 na kati yao, sita wana kesi ya kuhujumu uchumi.

**MIFUGO VS WATU**

Maise anakiri kuwapo tishio la ongezeko la mifugo na watu, linalochangia kilimo na malisho ya mifugo kuvamia eneo la hifadhi inayozaa mivutano ya kisheria kuhusu haki stahiki.

Diwani wa Mwada, Gerald Chembe, anasema mgogoro wa mazao kuliwa na mifugo na wanyamapori upo, huku akitaja kikwazo cha kisheria wanyama kama pundamilia kutoingizwa kwenye orodha ya wanaolipwa fidia.

"Imefikia mahali simba anaingia kwenye boma anakula ng'ombe. Kwa msimu huu, kuna watu mahindi yameliwa na pundamilia, ila kwa mujibu wa sheria, hawana fidia," anasema.

**HUJUMA KWA ASKARI**

Mbali na msuguano wa hujuma za kiuchumi na kijamii kati ya wanyama na binadamu, wakazi jirani, walinda usalama askari nao wana malalamiko katika eneo hilo.

Diwani Chembe anasema, Baraza la Maliasili Babati, liliamua wavamizi wa eneo oevu waondolewe na askari walipokwenda kutekeleza amri hiyo inayokaidiwa, baadhi yao walihudhuriwa kwa mikuki, akigusia tukio mojawapo la Machi mwaka huu.

Pia, anakumbusha tukio lingine la mwezi uliofuata Aprili mwaka huu, askari walipothubutu kuwaondoa waliovamia hifadhini, baadhi walipata madhara makubwa.

Katibu wa jumuiya hiyo, Maise, anasema mbinu wanayotumia wenyeji hao kutoka jamii za kifugaji, ni kujiunda kwa mfano wa kikosi kazi dhidi ya askari wanaothubutu kutetea mali za hifadhi.

"Uamuzi ulikuwa wavamizi kuondoka kwenye ardhi oevu iliyotolewa na vijiji vingine... vijiji ambao eneo lao lilivamiwa na kuharibiwa, vilinyimwa mgao na mwaka 2018 walipata nusu ya mgao," anasema.

**BURUNGE INAKOELEKEA**

Makamu Mwenyekiti wa Burunge WMA, Emmanuela Willium, anasema mpango mkakati wa baadaye ni kutengeneza eneo la utalii katika Mlima wa Oridoi, ili mgeni akiwa juu alione pia eneo lote la WMA.

Anasema kuwa pia watatengeneza kambi za kulala wageni ambazo zitamilikiwa na WMA nje ya zile za wawekezaji waliopo kwa sasa.

Willium pia anadokeza mpango wa kuanzisha shughuli za utalii kama vile mbio za mitumbwi kwenye Ziwa Manyara na Burunge ili kuongeza mapato zaidi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiifariji familia ya aliyekuwa mwanasiasa mkongwe nchini, marehemu Balozi Job Lusinde, eneo la Kilimani, jijini Dodoma, jana. Kutoka (kushoto) ni mjane Sarah Job Lusinde, mtoto wa marehemu, Dk. Mahewa Job Lusinde na Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela. **PICHA: OWM**

# Hamad Rashid ajinadi kwa kero za Muungano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa ADC, Hamad Rashid Mohamed, amechukua fomu ya kuomba kuwania urais wa Zanzibar kupitia Chama hicho ikiwa ni mara ya pili kugombea nafasi hiyo.

Mwaka 2015, aligombea nafasi hiyo lakini kura alizopata hazikumpatia ushindi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kuchukua fomu hiyo, Hamad alisema miongoni mwa mambo atakayohakikisha anayapatia ufumbuzi akipata ridhaa ya kuwa urais, ni kutatua kero za Muungano.

Hamad ambaye ni Waziri wa Afya wa Zanzibar, alisema kuna baadhi ya kero za Muungano ambazo Wazanzibari kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamikia, lakini baadhi hadi leo bado hazijapata ufumbuzi, hivyo ni imani yake kwamba akipata ridhaa zitaondoka.

Alisema vipaumbele vyake vingine ni kujadiliana na serikali ya Muungano kutoa urais wa nchi mbili kwa wale wenye kutaka hivyo, akidai kuwa lengo ni kuona maendeleo ya nchi yanapatikana.

Kuhusu elimu, alisema miongoni mwa mambo atakayosimamia ni kulipia mwaka wa mwanzo wa masomo kwa wanafunzi wote hata waliokosa mikopo, kutenganisha wanaume na wanawake katika shule yaani wanaume wawe na madarasa yao na wanawake vivyo hivyo.

Alisema hivi sasa wanafunzi wengi wa Zanzibar shule wanazosomea mazingira yake hayako salama katika majengo, hivyo atakapopata ridhaa ya kuongoza Zanzibar itakuwa na shule za ghorofa.

Licha ya serikali ya Zanzibar kuweka suala la elimu bure kwa ngazi ya msingi mpaka ualimu, chama chake kimeandaa utaratibu wa kuweka hadi shahada ya kwanza kuwa bure kwa wanafunzi wote.

# Meya Dar ajitosa urais CHADEMA

**Na Mary Geofrey**

ALIYEKUWA Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita, amejitosa katika kinyang'anyiro cha kuomba kuteuliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kugombea urais.

Mwita amekuwa mwanachama wa tano kujitokeza kuchukua fomu kutaka kupeperusha bendera ya chama hicho katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Alichukua fomu hiyo jana ikiwa ni miezi sita baada ya kung'olewa umeya wa jiji hilo Januari 9, mwaka huu, kwa madai mbalimbali ikiwamo tuhuma za matumizi mabaya ya gari la umma kwa kulisababishia kupata ajali.

Tuhuma nyingine zilizomfanya Mwita avuliwe umeya wa jiji hilo ni kushindwa kuongoza kikao cha Baraza la Madiwani na kupendelea baadhi ya mameya kuingia katika kamati za fedha.

Mwita alijitokeza katika ofisi za CHADEMA, jijini Dar es Salaam na kukabidhiwa fomu hiyo na Mkurugenzi wa uchaguzi wa chama hicho, Reginald Munisi.

Baada ya kuchukua fomu hiyo, Mwita aliahidi kuwa endapo chama chake kitampa ridhaa ya kuwania nafasi hiyo, kitu cha kwanza kwenye utawala wake ni kupatikana kwa Katiba Mpya kwa manufaa ya Watanzania wote.

"Katiba Mpya ndilo jambo la kwanza nitakaloanza nalo endapo chama changu kitaniamini na kunipitisha na hatimaye kuwa Rais wa Tanzania. Katiba itaheshimiwa na kila mtu," alisema Mwita.

Pia alisema atashughulikia tatizo la ajira kwa vijana nchini ambalo linasababishwa na mipango mibaya ndani ya serikali.

Alisema njia atakazotumia kuongeza ajira nchini ni kutumia sekta ya kilimo kuwekeza kilimo cha kisasa kitakachoajiri vijana wengi nchini.

"Endapo chama changu kitanipitisha kugombea urais nitaifanya kazi hii ya kusaidia Watanzania wengi kupata ajira kwa sababu hadi sasa ajira nyingi za wahitimu wa vyuo hazijatoka na Serikali imeshindwa kutumia mbinu za kutatua changamoto hii," alisema Mwita.

Kadhalika aliahidi kuwa, atatumia uzoefu wake wa kuliongoza Jiji la Dar es Salaam lenye watu zaidi ya milioni saba, kuliunganisha Taifa na kuleta watu pamoja.

"Nyie waandishi ni mashahidi nimekuwa nikitumia burasa kuongoza jiji hili na naamini nitatumia busara hizo kulileta taifa pamoja," alisema Mwita.

Mwanasheria wa CHADEMA, Tundu Lissu ndiye alikuwa mwanachama wa kwanza kuchukua fomu hiyo Julai 4, kupitia wakala wake David Jumbe. Dk. Mayrose Majinge alikuwa wa pili, alichukua fomu juzi Julai 7, mwaka huu.

Wengine waliochukua fomu hizo juzi ni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu na Wakili Gasper Mwanalyela.


ACB
AKIBA COMMERCIAL BANK PLC

**TAARIFA YA KUAHIRISHWA KWA MKUTANO MKUU WA MWAKA KWA WANAHISA WA AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**

**Kwa Wanahisa wote wa Akiba Commercial Bank Plc**

Notisi hii imetolewa kuwataarifu kuwa mkutano mkuu wa mwaka wa Wanahisa wa Akiba Commercial Bank Plc uliopangwa kufanyika **Jumamosi ya tarehe 25/07/2020** umeahirishwa kwa hivi sasa.

**Maelezo zaidi kuhusiana na kikao yatatolewa baadaye.**

n158053

www.acbtz.com
benki kwa maendeleo yako

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali iangalie wajane kunyang'anywa ardhi

**WANAHARAKATI** pamoja na makundi mengine ya utetezi wa haki za binadamu pamoja na mambo mengine, yamekuwa yakielekeza nguvu zaidi kupambana na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Kwa hakika matukio ya udhalilishaji yanaofanywa na baadhi ya wahalifu katika jamii dhidi ya makundi haya umeifanya ajenda ya utetezi iwe ya kudumu.

Tunakubaliana na tunaunga mkono kwa dhati jitihada zote zinazochukuliwa na watetezi hao dhidi ya wanawake na watoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia, kwa sababu vimekuwa vikichangia kundi la wanawake kuendelea kubaki nyuma kimaendeleo.

Aidha, vitendo hivyo vinawaathiri sana watoto hususan watoto wa kike na kuwakwamisha kushindwa kutekeleza ndoto zao za baadaye; kwa maana ya kuishia njiani kielimu kutokana na mimba pamoja na ndoa za utotoni.

Lakini suala la watoto wa kike kutopewa kipaumbele katika fursa ya elimu pia limekuwa likipigiwa kelele hivyo kuwa ajenda kubwa kwa watetezi na wanaharakati.

Sisi Nipashe tunaunga mkono kwa dhati jitihada hizo za utetezi wa makundi hayo, lakini tunaona kuwa kuna haja kwa watetezi hao kuliangalia kwa jicho la pekee suala la wajane kukudhalilishwa na kufanyiwa ukatili wa kunyang'anywa mali zao hususan ardhi, baada ya kufiwa na waume zao.

Suala hili ni changamoto kubwa kwa sasa katika jamii nyingi kwenye maeneo kadhaa nchini. Siyo rahisi kuyataja maeneo yote, lakini ni changamoto kubwa ambayo inakosesha haki wajane wengi.

Kwa mfano, wajane katika kijiji cha Sombanyasoko, wilayani Tarime, mkoani Mara, wamemwomba Rais John Magufuli kuwasaidia warudishiwe mashamba yao zaidi ya ekari 80 ambazo wanadai kunyang'anywa.

Wajane hao walidai kuwa maeneo hayo waliachiwa na waume zao kabla ya kufariki, na kwamba wamehangaika kutafuta haki hadi mahakamani, lakini wameshindwa kwa madai ya kuwapo vitendo vya rushwa. Mgogoro huo ambao umedumu kwa muda wa miaka saba, pia unahusisha familia nyingine nne.

Mmoja wa wajane hao, alidai wamenyang'anywa mashamba yao baada ya kuingizwa katika mgogoro wa ardhi ekari sita za watu watatu ambao walikuwa wanashtakiwa katika Baraza la Ardhi la Kata.

Alidai kuwa watu hao walikuwa wanashtakiwa kwa madai ya kumiliki ardhi ekari sita ambayo siyo mali yao.

Alidai katika kesi hiyo mlalamikaji alishindwa baada ya hukumu ya baraza hilo kutoa haki kwa washtakiwa na baada ya hukumu hiyo alikata rufani Baraza la Ardhi, Wilaya ya Tarime.

Imedaiwa na walalamikaji wengine kuwa katika uendeshaji wa rufani hiyo, mahakama haikuzingatia utaratibu wa kusikiliza na kutatua kesi za ardhi ikiwamo kufika eneo lenye mgogoro.


Pia, alidai washtakiwa hawakuitwa mahakamani kutoa ushahidi na Baraza la Ardhi la Kata halikushirikishwa kutoa maelezo yao.

Malalamiko ya wajane hao na mengine yanayotolewa katika maeneo mengine nchini, yanatoa picha kwamba pamoja na kuwapo na mamlaka kadhaa za kushughulikia mashauri ya ardhi, bado baadhi ya watu wanyonge wanaona kuwa hawatendewi haki.

Ushauri wetu ni kwamba kwa kuwa ardhi ni mali ya serikali chini ya Rais, tunaona kuwa kuna haja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwa na kitengo cha kufuatilia mashauri yaliyotolewa uamuzi na mabaraza ya ardhi na mahakama ili kama kuna yanayoonekana kuna na utata, yapelekwe kwa Rais aamue atakavyoona inafaa. Kwa kufanya hivyo tunaamini kuwa haki ya makundi ya wanyonge itapatikana.

Tunawashauri watetezi na wanaharakati kulitilia mkazo suala hili pia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Watumiaji wa methadone wabadilishe mazingira

**MATUMIZI** ya dawa za kulevya yamo katika orodha ya matatizo ya kitaifa, yanayoendelea kuikumba jamii, huku waathirika wakubwa wakiwa ni vijana. Ni taabu, kwani hao kimsingi, ndiyo wanaotegemewa nguvu kazi ya taifa.

Hata hivyo, serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali zikiwamo za uanzishaji msako dhidi ya wauzaji na waingizaji dawa hizo, ikiwa njia ya kukomesha matumizi ya dawa hizo nchini.

Mbali na hilo, imeanzisha nyumba za kutunza waathirika wa dawa hizo na pia kuanzisha vituo maalum, ambavyo waathirika wanaenda kunywa dawa za kuwawezesha kuachana na 'uteja' na wanapofikia nafuu, wanarudi nyumbani.

Hata hivyo, huenda juhudi hizo za serikali zisizae matunda kama inavyotarajiwa, kutokana na hali halisi inayowakabili 'mateja', hasa kuendelea kuishi kwenye mazingira yaliyosababisha wakajiingiza katika tatizo hilo.

Wengi wao ni wale walioshawishiwa kwenye vijiwe vyao na kujikuta wakutumia dawa hizo, na sasa wameamua kuacha na kuanza kutumia dozi ya dawa za kulevya, hivyo ni vyema wakaishi mazingira mengine.

Ninaamini kwamba kuendelea kuishi katika mazingira ya awali ni rahisi kushawishiwa kurudia matumizi ya dawa za kulevya, ambayo ni hatari kwa maisha yao.

Ipo haja ya kujenga nyumba nyingi kwa ajili ya watumiaji wa dawa hizo na walioamua kubadilika, ili wasiendelee kuishi katika mazingira ya awali, yanayoweza kuwarudisha kwenye hatari.

Pia, jukumu la kudhibiti vijana kujitumbukiza kwenye matumizi ya dawa, linaanzia katika ngazi ya familia, pia jamii haina budi kushirikiana katika kuelimisha, kuzuia, kurekebisha na kuwaponya waathirika wa dawa hizo.

Njia hiyo na ile ya kuwaondoa katika mazingira awali ni jambo muhimu kwa ajili ya kuwarejeshea utu na heshima yao kama binadamu ndani ya jamii, hasa wale wanaoamua kujitenga na uteja.

Ikumbukwe, mtu anapotumia dawa za kulevya na kisha akanywa methadone, ni rahisi kupoteza maisha, kwani hiyo ni kwa mujibu wa wataalamu wa afya wanaowatibu waathirika wa dawa hizo.

Dawa zote ni za usingizi, hivyo aliyeacha uteja akaitumia kisha akarudi 'kijiweni' na dawa za kulevya, anajiongezea usingizi mara mbili, hali ambayo ni hatari kwa uhai wake.

Hivyo wakati huu ambao serikali imefanikiwa kudhibiti matumizi ya dawa hizo nchini, kuna haja ya kuhakikisha wale ambao wameacha dawa hizo hawapati mwanya wa kurudia tena, bali wawe mabalozi wema kwenye jamii.

Pamoja na hayo, wale ambao wamekuwa wakitafuta mbadala wa dawa hizo wadhibitiwe ili warudi kwenye mstari, badala ya kuhangaika huku na huko kwa lengo la kuendelea na uteja.

Ninasema hivyo, kwa sababu baadhi ya vijana wanadaiwa kutumia gundi na dawa tiba zenye asili ya kulevya kama njia mbadala ya dawa za kulevya, ambazo kwa kiasi kikubwa zimedhibitiwa nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana, Sera na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, anasema hayo wakati akizungumza na wana habari katika Siku ya Maadhimisho ya Kupiga vita Dawa za Kulevya.

Anasema, tatizo la dawa za kulevya katika jamii ni mtambuka, linalohitaji ushirikiano wa sekta mbalimbali kwa ajili ya kupambana nalo, kwa vile udhibiti wa dawa hizo, umesababisha watumiaji kuhamia kwenye bhangi, mirungi, gundi na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

"Matumizi ya gundi ni eneo ambalo limewekewa mkakati maalumu; tumegundua watoto wanatumia, kimsingi tunaangalia uwezekano wa kuweka utaratibu ili matumizi ya gundi yadhibitiwe na isitumike kinyume," anasema.

Lakini inaelezwa kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na jumla ya waathirika wa dawa za kulevya kati ya 200,000 hadi 350,000, kwamba, kati yao waathirika takribani 30,000 wanatumia dawa hizo kwa kujidunga.

Wiziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Ummy Mwalimu ndiye anayesema hayo wakati akizindua kituo cha muda cha kutoa huduma ya Methadone kwa waraibu wa dawa aina ya heroin mkoani Tanga.

Kwamba, kuna makadirio ya asilimia 35 ya kiwango cha maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwenye jamii ya waathirika hao, hivyo hiyo yote ni dalili tosha kuwa ipo haja ya kuchukua hatua zaidi kuokoa waathirika.

HABARI KITAIFA

# 'House boy' auawa madai ya kuua watoto wa bosi wake

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

WATOTO wawili wa familia moja wanadaiwa kuuawa na kijana wa kazi za ndani kisha na yeye kuuawa na wananchi waliokuwa na silaha mbalimbali. Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa moja usiku katika Kijiji Cha Kwazoka Wilaya ya Kipolisi Chalinze mkoani Pwani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema tukio hilo limefanywa na Yasin Abdalla (35), mfanyakazi wa ndani wa Wema Senzie ambaye aliwaua watoto wawili kwa kuwakata na mapanga na kumjeruhi mama yao, Saada Salehe (28).

Kamanda Wankyo aliwataja watoto waliouawa kuwa ni Rehema Makolo (5) mwanafunzi wa awali na Abubakar Makolo(6) darasa la kwanza, wote walikuwa wanasoma katika Shule ya Msingi Kwazoka.

Akielezea tukio hilo, alisema baada ya mtuhumiwa kufanya tukio hilo la mauaji, wananchi walimkamata na kumuhifadhi katika ofisi ya kijiji, na kuwa akiwa humo alivunja mlango na kukimbia, lakini wananchi walifanikiwa kumkamata na kumshambulia kwa silaha za jadi na kufariki papo hapo.

Kamanda huyo alisema majeruhi ambaye ni mama wa watoto hao, amelazwa katika Kituo cha Afya Mlandizii qkipatiwa matibabu, huku maiti zikihifadhiwa katika kituo hicho kusubiri taratibu za mazishi.

Kamanda alisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea, na kwamba taarifa za awali za kiuchunguzi kuhusiana na mauaji hayo zinaelezwa kuwa kulikuwa na ugomvi kati ya mama wa watoto hao na mtuhumiwa.

# Mwili wa Lusinde kuzikwa leo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWILI wa waziri pekee aliyekuwa amebaki katika baraza la kwanza la mawaziri wa Tanganyika chini ya Mwalimu Julius Nyerere, Balozi Job Lusinde, unatarajia kuzikwa leo jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa ratiba ya mazishi iliotolewa uongozi wa Mkoa wa Dodoma jana, mazishi hayo yatahudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na utazikwa katika eneo la Kikuyu jijini hapa.

Balozi Lusinde alifariki dunia Julai 7, mwaka huu akiwa na umri wa miaka 90 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili jijini Dar es salaam alikopelekwa kwa ajili ya matibabu baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Mwili wa marehemu uliwasili jana jijini hapa kwa ndege na kupokewa na ndugu na viongozi mbalimbali wakiongozwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Balozi Lusinde alikuwa miongoni mwa mawaziri 11 wa kwanza wa Tanganyika, na alishika nafasi mbalimbali ikiwamo mwaka 1961-1963 alipohudumu uwaziri wa serikali za mitaa, mwaka 1963-1965 Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mwaka 1965-1967 Waziri wa Mawasiliano, Ajira na Kazi, mwaka 1970-1974 Waziri wa Mawasiliano, Usafiri na Kazi na mwaka 1974-1975 Waziri wa Mawasiliano na Kazi.

Balozi Lusinde pia alikuwa miongoni mwa mawaziri walioshiriki kikamilifu matayarisho ya muungano na pia alishuhudia utiaji saini wa Hati za Muungano Aprili 22, 1964.

Katika nafasi za ubalozi, Mwaka 1975 aliteuliwa na Mwalimu Nyerere kuwa Balozi wa Tanzania nchini China. Alihudumu huko hadi Septemba 1984 alipoteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Kenya.

# Viongozi 11 UWT wasimamishwa uanachama CCM tuhuma rushwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini, kimewasimamisha uanachama viongozi 11 wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) wilayani humo, pamoja na Mjumbe wa mkutano mkuu wa CCM Taifa, baada ya kukamatwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wakituhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Akitoa tamko la kusimamishwa wanachama hao, Katibu wa Siasa na Uenezi, Shinyanga Mjini, Saidi Bwanga, alisema kamati ya siasa ndani ya chama hicho, imetoa uamuzi huo baada ya kutuhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Alisema chama hicho kila mara kimekuwa kikikaa vikao vya ndani na kuwaonya viongozi kutojihusisha na vitendo vya rushwa, hasa katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye uchaguzi mkuu wa kuchagua madiwani, wabunge, na rais, lakini viongozi hao wameonyesha utovu wa nidhamu wa hali ya juu.

"Viongozi wa UWT ambao tumewasimamisha uanachama kuanzia sasa ni Hulda Malsaba, Zulfa Hassani, Jackline Isalo, Elzabeth Hange, Moshi Ndugulile, Tabu Shabani, Happy Chikala, Elizabeth Buzwizwi, Elizabeth Benjamini, Tabu Saidi, pamoja na mjumbe wa Mkutano Mkuu CCM Taifa, Asha Makwaiya," alisema Bwanga.

"Uchuguzi wa TAKUKURU utakapokamilika na wakikutwa na hatia tutaona nini cha kufanya, wakiwa hawana hatia basi watarudishiwa uanachama wao, pia tunatoa onyo kwa viongozi wengine pamoja na watia nia, wajiepushe na vitendo vya rushwa katika kipindi hiki cha uchaguzi, tofauti na hapo hatua kali zitachukuliwa dhidi yao," aliongeza.

Katika hatua nyingine, aliwataja wanachama 10 ambao wametia nia ya kugombea ubunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, kuwa ni Stephen Masele ambaye anatetea kiti chake, Bandora Mrambo, Wilbert Masanja, Erasto Kwilasa, Severine Kilulya, Jonathan Manyama, Lidya Piusi, Marry Izengo, Dotto Joshua na Eunice Jackson.

Viongozi hao wa UWT na mjumbe wa mkutano mkuu CCM Taifa, Julai Mosi, walikamatwa na TAKUKURU mkoani Shinyanga, wakiwa na vitenge, shuka, pamoja na kandambili vinavyodaiwa kuwa ni rushwa kwa wajumbe wa UWT.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### UAMUZI WA SHAURI LA UKIUKAJI WA KANUNI ZA UTANGAZAJI DHIDI YA KWANZA BROADCASTING LIMITED T/A KWANZA ONLINE TV

**1.0 UTANGULIZI**

Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano imetoa uamuzi dhidi ya Kwanza Broadcasting Limited T/A Kwanza Online TV kwa kukiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018 na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018.

Mnamo tarehe 01 Julai, 2020 kituo cha Kwanza Online TV kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii (Instagram), ilikiuka Kanuni za Utangazaji kwa kuchapisha taarifa inayodaiwa kutolewa na Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania. Kwanza Online TV ilichapisha taarifa hiyo iliyojaa upotoshaji kwa jamii bila kutafuta usahihi na ukweli wa taarifa husika, na bila ya kuzingatia mizania ya Habari. Kwanza Online TV ilichapisha maudhui hayo yaliyokuwa katika mfumo wa picha mnato, ambayo yanadaiwa yanatoka Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania.

**2.0 MAELEZO YA UTETEZI YA KWANZA ONLINE TV**

Katika utetezi/maelezo ya kimaandishi yaliyowasilishwa mbele ya Kamati ya Maudhui, uongozi wa **Kwanza Online TV** uliiambia Kamati kuwa **Kwanza Online TV** inapinga mashtaka husika kwani **Kwanza Online TV** imetoa taarifa inayotimiza matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Ibara ya 18, inayompa mtu uhuru wa kutoa maoni yo yote, kutoa mawazo yake, kutafuta, kupokea, kutoa habari na dhana zo zote kupitia chombo cho chote bila kujali mipaka ya nchi.

Aidha, katika maelezo hayo, Uongozi wa **Kwanza Online TV** uliiambia Kamati kuwa walichapisha habari hiyo kwa lengo la kuujulisha umma juu ya maoni ya Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania, kuhusu ugonjwa wa COVID-19. Uliendelea kudai kuwa, kwa asili ya habari hiyo ni kwamba haikuwa na mantiki wala haja ya kutafuta upande wa pili kwani taarifa hiyo ilikuwa ni taarifa kwa umma na siyo aina ya taarifa ambayo inahitaji upande wa pili kwa sababu yale yalikuwa ni maoni na msimamo wa Ubalozi wa Marekani, na hata kutafuta na kupata maoni ya upande wa pili kusingeweza kubadili maudhui ya taarifa ambayo imechapishwa na Ubalozi wa Marekani.

Hali kadhalika, uongozi wa **Kwanza Online TV** ulidai kuwa uzalendo wao ulikuwa ni kuujulisha umma kuwa mataifa mengine yanazungumza nini kuhusu nchi ya Tanzania, na ni hatua gani nchi yetu inatakiwa ichukue ili kuepuka minong'ono kutoka mataifa mengine.

Pamoja na utetezi wao, **Kwanza Online TV** walidai kuwa walipewa notisi ya kutoa maelezo yao ya utetezi chini ya saa 24.

**3.0 UAMUZI WA KAMATI**

Baada ya kupitia kwa umakini na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi wa maandishi uliotolewa na Uongozi wa **Kwanza Online TV,** Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **Kwanza Online TV** kupitia ukurasa wake wa mitandao ya kijamii wa ***Instagram*** imekiuka Kanuni Na. 7(1) (a), (b) na 12 (l) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018 pamoja na Kanuni Na. 11(1)(a) na 15(2)(b) na (c) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

**Hivyo basi,** kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2017, Kamati ya Maudhui inaamua kutoa adhabu ya kuifungia **Kwanza Online TV** kutotoa huduma kwa kipindi cha **miezi kumi na moja** (11) kuanzia tarehe **06 Julai, 2020,** ili waweze kujirekebisha.

**Taarifa hii imetolewa na:**
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Maudhui**
**06/Julai/2020**

215806002




Mwenyekiti wa Chama cha ADC Taifa, Hamad Rashid Mohamed (kulia), akikabidhiwa fomu ya kuteuliwa kugombea urais wa Zanzibar kupitia chama hicho na Mkurugenzi wa Mipango, Uchaguzi na Uendeshaji wa chama hicho, Omar Albert Costantine, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bil. 2.3/- zanunua vifaa uhitaji maalum

**Na Mwandishi wetu**

SERIKALI imesema kuwa imetumia zaidi ya Sh. bilioni 2.3 kununua vifaa vya elimu na saidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye uhitaji maalum wa shule za msingi 708 na sekondari 45 nchini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa usambazaji wa vifaa hivyo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dk. Ave Maria Semakafu, alisema fedha hizo zilitolewa kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Alisema vifaa hivyo vinalenga kuimarisha ujifunzaji wa wanafunzi wenye uhitaji maalum waliopo katika shule za msingi na sekondari nchini.

Dk. Semakafu alisema pamoja na kugawa vifaa hivyo, wizara iliendesha mafunzo kwa walimu wa lugha ya alama wanaofundisha shule za sekondari, ili waweze kutekeleza jukumu la ufundishaji ikiwa ni pamoja na kutengeneza kamusi ya lugha za alama ya kufundishia shule za msingi na sekondari.

"Tunashukuru maono ya serikali kwa kuwa imefungua fursa za elimu kwa kuondoa vikwazo vilivyokuwa vinasababisha watoto kufaidika na fursa hizo,"alisema

Naibu Katibu Mkuu alimtaka Mkurugenzi wa Elimu Maalum kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Magreth Matonya, kuwa na eneo la kipaumbele la kushughulikia kila mwaka kwa wanafunzi wenye uhitaji maalum.

Naye Dk. Matonya alitaja baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa kuwa ni mashine kubwa ya kuchapa maandishi ya wasioona, mashine 27 za kurudufu maandishi ya nukta nundu, mashine 60 za kupima kiwango cha usikivu na vifaa 60 vya kufundishia matamshi kwa wanafunzi wenye changamoto ya matamshi.

Vingine ni miwani 5,167 za kuzuia mionzi ya jua, vioo 2,067 vya kukuza maandishi kwa watoto wenye ualbino na uoni hafifu, vifani 5,720, abakasi 9,909, pazo 2,260 za kufundishia stadi za kujimudu na hisabati kwa watoto wenye ulemavu wa akili na wenye usonji pamoja na vitimwendo kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa viungo.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Maulid Maulid, alimhakikishia Naibu Katibu Mkuu kuwa vifaa hivyo vitafika shuleni kwa wakati na vitatumika ipasavyo badala ya kufungiwa stoo.

# Wajane wamlilia JPM wakidai kunyang'anywa ardhi

**Na Happy Severine,** TARIME

WAJANE sita katika kijiji cha Sombanyasoko, wilayani Tarime, mkoani Mara, wamemuomba Rais John Magufuli, kuwasaidia warudishiwe mashamba yao zaidi ya ekari 80 ambazo wanadai kunyang'anywa.

Wajane hao walidai kuwa maeneo hayo waliachiwa na waume zao kabla ya kufariki na kwamba wamehangaika kutafuta haki hadi mahakamani, lakini wameshindwa kwa madai ya kuwapo vitendo vya rushwa.

Mgogoro huo ambao umedumu kwa muda wa miaka saba, pia unahusisha familia nyingine nne.

Mang'era Nyaswi mmoja wa wajane hao, alidai wamenyang'anywa mashamba yao baada ya kuingizwa katika mgogoro wa ardhi ekari sita za watu watatu ambao walikuwa wanashtakiana katika baraza la ardhi la kata.

Nyaswi alidai kuwa wananchi hao, Daniel Chacha na Meng'anya Magoti, walikuwa wanashtakiwa na Mseti Gachuma kwa madai ya kumiliki ardhi ekari sita ambayo siyo mali yao.

Alidai katika kesi hiyo Gachuma alishindwa baada ya hukumu ya baraza hilo kutoa haki kwa washtakiwa na baada ya hukumu hiyo Mseti alikata rufani Baraza la Ardhi, Wilaya ya Tarime.

Naye Sulemani Magoti alisema kuwa katika uendeshaji wa rufani hiyo, mahakama haikuzingatia utaratibu wa kusikiliza na kutatua kesi za ardhi ikiwamo kufika eneo lenye mgogoro.

Pia, alidai washtakiwa hawakuitwa mahakamani kutoa ushahidi na baraza la ardhi la kata halikushirikishwa kutoa maelezo yao.

Loyce Daudi, alidai baada ya hukumu ya Baraza la wilaya, mlalamikaji alikwenda na madalali na badala ya kuchukua ekari sita, walishangaa kuchukua mashamba mengine yakiwamo ekari 80 za kwao.

Naye Gati Mwita, alisema kuwa mashamba yao walipewa zamani toka mwaka 1970 waliyokabidhiwa na serikali ya kijiji kwa nyaraka, ambazo mpaka sasa zipo na ndizo zilitumika kwenye baraza la ardhi la kata.

Wajane hao na familia hizo nyingine walimuomba Rais Magufuli kuwasaidia wapate haki yao kwa kuwa wamehangaika mpaka ofisi ya Mkuu wa Wilaya, lakini hawajasikilizwa.

Aliyekuwa Katibu wa Baraza la ardhi la kata wakati wa kesi ya awali ya watu watatu, Ezekiel Magondo, alisema walitoa ushindi kwa washtakiwa baada ya kujiridhisha na vielelezo vyao na kufika eneo la mgogoro.

"Baraza lilibaini kuwa mlalamikaji hakuwa na haki na lile eneo la ekari sita, na kesi yake toka awali mpaka anakata rufaa alilalamikia ekari sita na siyo hizo nyingine za wajane na wananchi wengine zaidi ya 74," alisema.

Mwenyekiti wa kijiji, Chacha Fanusi, alikiri kuwapo kwa mgogoro huo, huku akishangaa kuona maeneo ya wajane hao yakichukuliwa wakati hawakua katika kesi.

Ofisa Ardhi wa halmashuari ya wilaya hiyo, Privatus Mafuru, alikiri kuwapo kwa mgogoro huo na tayari ofisi yake imetoa maelekezo kwa walalamikaji wafike ofisini wakiwa na vielelezo vyote ili wasaidiwe.

Alisema tangu awape maelekezo hayo wananchi hao hawajarudi ofisini kwake kuleta nyaraka hizo ikiwamo hukumu hali ambayo inamfanya ashangae kuona wanalalamika.

# 15 kutoa ushahidi kesi dhidi ya Idriss

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri umesema unatarajiwa kuita mashahidi 15 dhidi ya msanii Idriss Sultan (27) na Innocent Maiga, wanaokabiliwa na kesi ya kushindwa kusajili laini ya simu inayomilikiwa na mtu mwingine.

Kesi hiyo imepangwa kuanza kusikilizwa ushahidi Agosti 5, mwaka huu.

Awali, mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu, ilisikiliza maelezo ya awali ya washtakiwa.

Wakili wa Serikali, Silvia Mitanto, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Alidai kuwa kati ya Desemba Mosi, 2019 na Mei 19, 2020 katika eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, Idriss alitenda kosa la kushindwa kufanya usajili wa laini ya simu inayotumiwa na mtu mwingine.

Ilidaiwa kuwa katika kosa hilo mshtakiwa alitumia kadi ya simu iliyomilikiwa na Innocent Maiga bila kuripoti kwa mtoa leseni.

Katika shitaka la pili, mshtakiwa Maiga anadaiwa kutenda kosa la kushindwa kutoa taarifa ya mabadiliko ya kadi ya simu kutoka kwake kwenda kwa Idriss, kosa analodaiwa kulitenda kati ya Desemba Mosi, 2019 na Mei 19, mwaka huu, eneo la Mbezi Beach, Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Pia alidai Mei 5, mwaka huu, Mkuu wa Upelelezi Kinondoni, alipewa taarifa kwamba Idriss anatumia kadi ya simu ya Vodacom ambayo haijasajiliwa kwa jina lake na kwamba alitakiwa kuripoti Kituo cha Polisi Oysterbay na alifanya hivyo.

Ilidaiwa polisi walienda kufanya upekuzi nyumbani kwa Idriss na kubaini uwapo wa laini hiyo ya simu aliyokuwa akiitumia kwa mawasiliano yake ya kila siku licha ya kusajiliwa kwa jina la Maiga.

Ilidaiwa Idriss aliakiri kutumia kadi hiyo ya simu ambayo ilikuwa ikimilikiwa kabla na Maiga na kwamba alikiri kuitumia tangu Desemba, mwaka jana.

Maiga alidaiwa kukiri kumiliki kadi hiyo na alimpatia Idriss aweze kuitumia na alikiri kutoripoti kwenye mamlaka kuhusu mabadiliko ya kadi hiyo.

Upande wa mashtaka ulidai utaleta mashahidi 15.

# Waajiriwa wapya sekta ya afya wafundwa

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Mabula Mchembe, amewataka waajiriwa wapya wa afya kufanya kazi kwa kufuata taratibu za kitaalamu na kuzingatia maadili ya utumishi.

Kadhalika, ameagiza wale wataalamu wa maabara kuhakikisha wanatoa vipimo ambavyo ni sahihi kwa wagonjwa.

Mchembe alitoa maelekezo hayo jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mradi wa kusaidia huduma za afya, ambapo wataalamu 575 wameajiriwa na Taasisi ya Benjamin Mkapa Foundation (BMF).

“Napenda kuwasihi kuwa ni vyema kuzingatia maadili ya utumishi na kujitahidi kuwa mfano katika maeneo yenu mtakayokuwa mkifanya kazi. Uadilifu wenu katika utoaji wa huduma ni wa muhimu kwani mtakuwa ni kioo cha namna sekta yetu ya afya inavyofanya kazi,” alisema Mchembe.

Aidha, alisema tangu serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani, jumla ya vituo vipatavyo 488 vimejengwa na kukarabatiwa. Idadi hiyo inajumuisha zahanati 76, vituo vya afya 320, hospitali za wilaya 22 na hospitali mpya za wilaya 25 na hospitali mpya za rufani za mikoa 5.

“Hospitali nyingine za wilaya 28 zipo katika ujenzi wa awamu ya pili. Idadi ya ongezeko la uhitaji wa huduma kutokana na vituo vilivyokarabatiwa na kujengwa linaongeza hitaji la rasilimali watu kwa kiwango cha asilimia tatu kwa mwaka,” alisema.

Mchembe alisema hadi kufikia juzi nchi ina jumla ya wataalamu wa afya 99,6841 kati ya wataalamu 209,6032 wanaohitajika.

Alisema hali hiyo ni kutokana na ongezeko la uhitaji wa huduma kwa jamii pamoja na maboresho ya huduma yanayoendelea kufanyika hasa upanuzi na ujengaji wa vituo vya kutolea huduma.

Aidha, alisema licha ya uhaba wa watumishi kwa kiwango, pia kumekuwa na uwiano usio sawa wa upangaji wa watumishi katika maeneo ya kutolea huduma.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa BMF, Dk. Ellen Senkoro, alieleza kwamba wataalamu wa afya hao 575 wamependekezwa kupangwa katika maeneo yaliyopewa kipaumbele na serikali katika kuongeza nguvu ya kuimarisha huduma za afya za kupambana na magonjwa ya maambukizi na yasiyo ya maambukizi.

“Napenda kuchukua fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wizara ya Afya na TAMISEMI kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa katika kufanikisha zoezi hili muhimu,” alisema.

Alisema kufika Juni 2020, BMF iliajiri jumla ya wataalamu wa afya 3,004 na kati yao 1,064 wamehuishwa katika utumishi wa umma.




Maofisa mauzo wa kampuni ya Lake Gas, Mohamed Mguwa na Wema Msami, wakimpa maelezo mwananchi kuhusu ubora wa bidhaa zao katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kwenye Viwanja wa Mwalimu Nyerere, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maofisa ugani waagizwa elimu kilimo cha kisasa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imewagiza maofisa ugani wa halmashauri zote za mkoa huo kushirikiana na wataalamu pamoja na watafiti wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) katika kutoa elimu ya kilimo cha kisasa.

Kilimo hicho kilenga kuzalisha mazao mengi katika eneo dogo la ardhi, ili kuongeza tija kwa wakulima, ambao wataondokana na migogoro ya kugombea ardhi.

Agizo hilo limetolewa na Katibu Tawala wa Mkoa huo, Emmanuel Kalobelo, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wakulima ya mradi wa Shirika la Jitihada Shirikishi za kuleta mapinduzi ya kilimo vijijini, katika kukabiliana na njaa na umaskini (RIPAT-SUA) yaliyofanyika Kijiji cha Mlali, wilayani Mvomero.

Wakulima wa vikundi vipatavyo 22 wamenufaika kufundishwa kilimo bora na matumizi ya teknolojia ya kisasa na watafiti wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Insia ya SUA kupitia mradi wa RIPAT-SUA chini ya ushirikiano na Shirika la RECODA.

Kalobelo alisema elimu iliyotolewa na mradi huo licha ya wakulima kupata mazao mengi katika eneo dogo la ardhi, pia teknolojia hiyo inasaidia kupata mazao bora tofauti na yanayopatikana kwa kutumia kilimo cha kawaida.

Alisema ni vema maofisa ugani wa kila halmashauri ya wilaya za mkoa huo kuchukua elimu hiyo inayotolewa kupitia RIPAT-SUA na kwenda kuisambaza kwa wakulima katika halmashauri zao.

Alivitaka vikundi vya wakulima kutumia teknolojia ya kilimo waliyoipata kupitia miradi mbalimbali inayofadhiliwa kupitia SUA na sehemu nyingine kuwa ni nyenzo madhubuti kwao na jamii inayowazunguka badala ya teknolojia kuitelekeza mara mradi unapokoma.

“Tuna tatizo sisi Watanzania, wakati mwingine tunafundishwa kweli na tunajifunza kweli, lakini tukisha toka hapa inakuwa kama maigizo... sasa tusifanye elimu tuliyoipata hapa iwe ya maigizo, twendeni tukaifanyie kazi,” alisisitiza Kalobelo.

Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, Prof. Raphael Chibunda, alivitaka wanavikundi vilivyopo kwenye mradi huo kuacha mazoea ya kutelekeza teknolojia wanayopata kwa maagizo pia aliwataka watafiti na wataalamu wa chuo hicho kuongeza kasi ya kuwasaidia kikamilifu wakulima badala ya kufanya utafiti wa kimazoea.

Naye Mratibu wa Mradi huo, Dk. Emmanuel Malisa, alisema mradi wa RIPAT unafadhiliwa na Denmark ambao ulianza mwaka 2018 ukikusudia kusaidia jamii kukabiliana na njaa na umaskini.

## Wakazi B’moyo walia kukosekana kwa maji

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WAKAZI wa Kijiji cha Mkenge, wilayani Bagamoyo ambao ni jamii ya wafugaji wamelalamikia adha ya maji inayowakabili kwa muda mrefu na kusababisha kutumia muda mwingi kufuata huduma hiyo.

Hali hiyo imefanya baadhi ya wakazi wa kijiji hicho kukwama kuendelea na shughuli za ufugaji kutokana na kutumia muda mwingi kutafuta maji maeneo ya Magogoni na Kaloleni.

Mmoja wa wakazi hao, Esther Malimengi, alisema kutokana na kukosekana kwa huduma hiyo, kijiji chao kimekwamishwa kuendeleza shughuli za ufugaji na kilimo na kuwafanya kudumaa kimaendeleo.

Aliomba serikali kuingilia kati suala hilo ili nao wapate maji ya bomba na kufanya shughuli zao za uchumi kama ilivyo katika maeneo mengine.

Naye Simon Mobitu, alisema kutokana na changamoto hiyo wanaume wamepunguza kupeleka mifugo kwenye malisho ili waweze kupata muda wa kusaka maji na kazi ya mifugo kuwaachia watoto.

## Bosi Benki ya NCBA aahidi huduma bora

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mkuu Mteule na Ofisa Mtendaji Mkuu Mteule wa Benki ya NCBA, Margaret Karume, ameahidi kuwa benki hiyo itatoa huduma nzuri na za viwango.

Aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa huduma za benki ya NCBA ikiwa ni muunganiko kwa benki mbili ambazo ni NIC na CBA.

Karume alisema mwezi mmoja baada ya uzinduzi huo watabadilisha alama kwenye matawi yao na taarifa ili kuakisi utambulisho wa benki hiyo.

“Muungano huu unafanya benki hii kwa sasa iwe kwenye daraja la pili katika taasisi za kibenki inayotoa huduma na bidhaa pana ikijipatia nguvu kutoka benki zilizopita,” alisema.

Pia alisema kwa sasa benki hiyo ipo katika hatua ya mwisho za uunganishaji wa mifumo ili wateja waendelee kufurahia huduma kirahisi kwenye nyanja zote nchini.

“Lengo letu hadi robo tatu ya mwaka huu, wateja wote wa NCBA wapate huduma sawa na za kiwango bila kujali mahusiano ya zamani ya NIC na CBA,” alisema Karume.

## Standard Chartered yaisaidia Red Cross, UNICEF bil. 1.2/-

**Na Enock Charles**

BENKI ya Standard Chartered Tanzania imetoa Sh. bilioni 1.2 kwa Chama cha Msalaba Mwekundu (Red Cross) Tanzania na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Watoto (UNICEF) kwa ajili ya kusaidia shughuli mbalimbali ikiwamo elimu na afya.

Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Sanjay Rughani, alisema katika taarifa kuwa kati ya dola 550,000 zilizotolewa na benki (sawa na shilingi bilioni 1.265) kati dola 300,000 zimegawiwa kwa Red Cross na dola 250,000 kwa UNICEF.

"Benki ya Standard Chartered inajivunia kuchangia fedha kwa ajili ya mipango mbalimbali ya Red Cross Tanzania na UNICEF, hivyo kusaidia makundi yaliyo katika mazingira hatarishi," alisema Sanjay.

Alisema benki imekuwa ikifadhili shughuli mbalimbali za kusaidia wananchi hasa katika mabara ya Asia na Afrika kama ya afya, mawasiliano, miradi ya elimu ili kuzisaidia nchi za mabara hayo.

Alisema Red Cross ambayo inafanya kazi maeneo mbalimbali duniani, itasaidia kutolewa kwa huduma za afya katika shule za msingi na sekondari maeneo mbalimbali duniani, mawasiliano, kutoa mavazi maalum ya kujikinga na maradhi hasa kwa wataalamu wa afya wa kujitolea na waajiriwa pamoja na kutoa huduma ya chakula kwa waathirika wa virusi vya corona.

## Andengenye awaonya watumishi kuhusu rushwa

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, amewataka watumishi wa serikali na wakazi wa mkoa huo kuacha kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Alitoa rai hiyo wakati akizungumza na watumishi wa Mkoa wa Kigoma wakati wa makabidhiano kati yake na mtangulizi wake, Emmanuel Maganga na kwamba rushwa ni adui wa haki, hivyo kuwataka watumishi kuhakikisha hawajihusishi na vitendo hivyo.

Andengenye alisema: "Mafanikio yote tuliyoyafanya kama tutashindwa kudhibiti rushwa yatabomoka, naomba tuungane na hilo, kwa sababu rushwa itatucheleweshea maendeleo."

Alisema dhamana ya watumishi waliyonayo haiwezi kupimwa kwa mshahara, inapimwa kwa heshima na dhamana kubwa waliyopewa.

Kwa upande wake, Maganga aliwataka wananchi wa mkoa huo kumwombea ili aweze kufanikisha mbio zake za ubunge katika Jimbo la Mvomero.

# Lukuvi awashukia viongozi uporaji ardhi

**Na Munir Shemweta,**
KATAVI

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amekerwa na tabia ya baadhi ya viongozi kuhusika kupora ardhi ya wananchi, akionya kuwa dawa yao iko jikoni.

Amesema tabia hiyo iko mbioni kukomeshwa kutokana na watendaji wa sekta ya ardhi kuhamishiwa wizarani sambamba na kuanzishwa ofisi za ardhi katika mikoa. Waziri Lukuvi alisema hayo juzi wakati wa kuzindua ofisi ya ardhi Mkoa wa Katavi wilayani Mpanda, ikiwa ni mfululizo wa uzinduzi wa ofisi za ardhi kwenye mikoa mbalimbali nchini. Alisema wapo baadhi ya viongozi wa wilaya na mkoa ambao ni sehemu ya migogoro ya ardhi na wamekuwa wakitumia madaraka yao vibaya kwa kupora na kuuza ardhi ya wananchi.

Lukuvi aliweka wazi kuwa tabia hiyo inamkera Rais John Magufuli na katika kushughulikia tatizo hilo, wameona kuna haja ya kuchukua hatua kwa kuanzisha ofisi kila mkoa.

Kwa mujibu wa Lukuvi, uanzishwaji ofisi za ardhi za mikoa pamoja na uhamishaji watendaji wa sekta ya ardhi kutoka Tamisemi kwenda Wizara ya Ardhi, kunatoa nguvu kwa watumishi wa sekta ya ardhi kutumia na kusimamia sheria.

"Kuna viongozi wa kuchaguliwa na wa kuteuliwa wanaotumia madaraka yao vibaya kwa kupora ardhi ya wananchi. Safari hii hakuna fursa hiyo maana watendaji wote wa sekta ya ardhi wako chini ya Wizara ya Ardhi, madiwani hawawezi tena kuazimia kuwafukuza," alisema. Akizungumzia upimaji ardhi katika Mkoa wa Katavi, Lukuvi aliagiza hadi kufikia mwisho wa mwaka huu, vijiji vyote katika mkoa huo viwe vimepimwa na kupatiwa hati za kijiji sambamba na wamiliki 15,000 waliokwama kupewa hati kutokana na urasimu, kupatiwa hati zao.

Alisema kuwa kwa sasa, hakuna visingizio vya kuchelewa kutoa hati hizo kwa kuwa vifaa kwa ajili ya upimaji vipo.

Lukuvi aliuagiza mkoa huo kupima ardhi na kutoa hati baada ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Katavi, Siyabumi Mwaipopo, kusema kuwa kati ya vijiji 172 vilivyoko kwenye mkoa huo, vijiji vitatu tu vilivyopimwa na kupatiwa hati za vijiji.



Mafundi wakijenga mifereji ya maji machafu katika eneo la Serengeti Chang'ombe, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Faini 500,000/- kwa kumiliki kobe bila kibali

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemuhukumu Daniel Chizuwa kulipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela miaka miwili baada ya kukutwa na hatia ya kosa la kumiliki nyara za serikali ikiwamo kobe wawili bila kibali.

Chizuwa alihukumiwa adhabu hiyo jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Awali, mshtakiwa alikiri kosa la kujihusisha na nyara za serikali bila kibali baada ya kuingia kwenye makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP).

Pamoja na adhabu hiyo, tayari mshtakiwa huyo ameshalipa sehemu ya makubaliano hayo Sh. 650,000.

Kabla ya kupewa adhabu hiyo, Wakili wa Serikali Ladislaus Komanya, aliieleza mahakama kuwa mshtakiwa hana makosa ya nyuma na atatekeleza makubaliano aliyoingia na DPP, mahakama itoe adhabu kwa taratibu za kisheria.

Kwa upande wake mshtakiwa aliiomba mahakama isimpe adhabu kali kwa kuwa amejifunza kutokana na makosa, atakuwa balozi ili watu wengine wasitende makosa kama haya.

"Naomba mahakama inipe adhabu ndogo kwa sababu nina familia inayonitegemea," alidai

Katika kesi hiyo Chizuwa anadaiwa kuwa Januari 22, mwaka 2020 eneo la Masaki, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, alijihusisha na nyara za serikali kwa kukutwa na kobe wawili hai wenye thamani ya Dola za Kimarekani 140 sawa na Sh. 320,600 mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila leseni ya kumruhusu kuwa na nyara hizo kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.



Ukurasa 13

Ni ushauri tu kwa Rais JPM


Ukurasa 12

## Magereza imeingia darasa la mbegu bora, safari kujitosheleza chakula

BUFE
IJUMAA JULAI 10, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Sekta binafsi, wanaowajibika nayo waumiza vichwa safari endelevu

## • Kipato Kati; teknolojia kijani; haki jinsia

**Na Mwandishi Wetu**

TANGU zamani sekta binafsi imekuwa na mchango muhimu katika kutokomeza umaskini na kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Katika nchi zinazoendelea, sekta binafsi inatajwa kutoa nafasi za ajira tisa, kati ya 10 katika nchi zinazoendelea.

Ni sekta yenye majukumu muhimu ya kutekeleza katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu na kutatua matatizo ya dunia, ikileta ufanisi ulioboreshwa, matumizi ya teknolojia na uvumbuzi.

Katika semina iliyofanyika kwa njia ya mtandao yenye jina la 'Ustahimilivu wa Sekta Binafsi' ikilenga kuangalia jinsi uongozi wa pamoja unavyoweza kugeuza upotevu wa asili iliyofanyika jijini Dar es salaam.

Washiriki walikubaliana kila kampuni kwa kujitegemea, ikamate ajenda ya mazingira iliyoambatanishwa katika mpango wake wa uwekezaji jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom, Hisham Hendi, anasema kampuni hiyo ina falsafa na mchango katika kufikiwa maendeleo endelevu.

Anasema, uwajibikaji wa kampuni kupitia utendaji endelevu ni kipengele muhimu kwao na wametoa mwongozo kwa kila nyanja ya uwekezaji, utanuzi, ukuaji na utoaji wa huduma.

"Mkakati wetu wa kipindi cha kati unaendana vyema na Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa ya Mwaka 2016/2021 na malengo ya maendeleo endelevu ambayo yameanzishwa, kuhamasisha Tanzania kutambua mpango wake wa kuwa na jamii ya kipato cha kati kufikia 2025," anasema.

"Kazi yetu inaharakisha ujumuishwaji wa kifedha na kufanya kazi na makundi mbalimbali ya kijamii, makundi ya wanawake na vijana vile vile kusaidia kufikiwa SDG5 (usawa wa kijinsia)," anafafanua Hisham.



Shughuli za kuzalisha bidhaa samaki katika moja ya viwanda binafsi. **PICHA: MAKTABA.**

Naibu Mwakilishi mkazi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) nchini, Sergio Valdini, anahamasisha uimarishaji ushirikiano na sekta binafsi katika kufadhili na kuwezesha teknolojia ya kijani katika utendaji.

Balozi wa Norway nchini, Elizabeth Jacobsen, anasisitizia haja ya kuwapo juhudi zilizokubaliwa zinazohusu watendaji mbalimbali kuimarisha utendaji wa kibiashara katika uwajibikaji.

"Tunapaswa kuhamasisha jamii yenye uwazi na wadau mbalimbali kutekeleza majukumu yao katika majadiliano, kuhusu mazingira kwa lengo la kuchukua mawazo bora zaidi, kuhusu teknolojia ya kijani na ubunifu," anasema Elizabeth.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Bia Tanzania, Philip Redman, anasema dhana ya 'uendelevu' ni ya msingi kwenye biashara na sio kitu cha ziada, katika uhakikishaji kwamba mikakati uendelevu inasimikwa kama sehemu ya falsafa ya biashara.

Mchangiaji, Simon Shayo, Makamu Rais wa kampuni ya AngloGold Ashanti, anapongeza majadiliano hayo ya wazi ya wadau na ushirikiano uliopo kati ya mashirika ya kitaalamu kusaidia jitihada za serikali kuhakikisha ukuaji imara wa uchumi wa kijamii, hatimaye kuchangia kufikiwa malengo yote 17 endelevu.

Sekta binafsi inaendelea kuwa na jukumu muhimu katika kufadhili na kuwezesha jitihada nyingi za uendelevu za kiserikali, jambo linalotajwa kuleta mabadiliko chanya katika jamii, ikiwamo manufaa ya kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Ni semina iliyowaleta pamoja, viongozi kutoka taasisi mbalimbali za kibiashara na washirika wa maendeleo katika kuimarisha jitihada za pamoja.

Vilevile inatajwa kuwa mfano hao na mafunzo bora kuhusu jinsi ya kutumia mifumo yake katika kufikia malengo ya kibiashara na kuboresha maadili, utendaji salama kwa mazingira na kufadhili jitihada za kijani kuelekea kufikia malengo ya usawa wa kijinsia.

UCHUMI

## AGIZO LA KUJILISHA...

# Magereza imeingia darasa mbegu bora, safari kujitosheleza chakula

**Na Christina Haule, Morogoro**

BAADA ya agizo la Rais Dk. John Magufuli kutaka Magereza yote 129 nchini kujitosheleza kwa chakula, Jeshi la Magereza limeitikia hilo kwa kuchukua ya kujipanga kuzalisha mbegu bora, kwa mujibu wa elimu wanayoipata kutoka kwa wazalishaji wake.

Kamishna Msaidizi (ACP) wa Jeshi la Magereza Roswin Mbena, anasema jeshi hilo limepata mafunzo ya uandaaji na uzalishaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali, ili kukamilisha mikakati ya kujitosheleza kwa chakula.

Ni namna ACP Mbena, anaifafanua kwamba kuna haja ya Maregeza kujikita kwa wazalishaji na wauzaji wakubwa wa mbegu za mazao mbalimbali nchini.

Anasema kutokana na mafunzo waliopatiwa kuhusu namna ya kuzalisha mbegu bora, ujuzi walioupata kutoka Taasisi ya kudhibiti Ubora wa Mbegu nchini (TOSCI), yanayowasaidia.

Msingi wa tafsiri ya mbegu kitaalamu, ni sehemu ya tunda la mmea inayoweza kuendelea kuwa mmea mpya. Mbegu ni njia ya kuzaliana kwa mimea mingi zinazoitwa kwa lugha ya kibaiolojia 'spermatophytina'

Chanzo chake, kinaelezwa kuanzishwa ndani ya ua la mmea na inaendelea kukua. Zimegawanyika katika mbegu ndogo sana ambazo ni vigumu kuziona na mbegu kubwa.


TOSCI, msingi wake ina wajibu wa kuzalisha mbegu kuu; chotara na za kisasa kama za mazao mahindi na mtama.

Kwa mujibu wa ACP Mbena, asasi hiyo inawaimarisha katika uzalishaji mbegu na hatimaye kupata mazao yenye ubora na viwango vinavyokubalika kitaifa.

Ofisa huyo mwandamizi wa kijeshi, anasema wameshaanza kutekeleza mikakati iliyowekwa na Magereza, wakianza na elimu ya namna ya kuandaa na kuzalisha mbegu bora za mazao kutoka TOSCI.

Hiyo inafanyika katika azma ya kufanikisha uzalishaji wa mbegu bora kutoka kwenye mashamba yao yote ambayo zaidi ya ekari 12,000.

Anasema, jeshi hilo limekuwa likijihusisha na kilimo cha mazao mbalimbali katika mashamba hayo, ikiwamo miti, mazao ya biashara, chakula na bustani, lakini wameshindwa kufikia malengo ya uzalishaji, kutokana na kununua mbegu kwa wazabuni ambazo hazina ubora unaostahili.



Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Ubora wa Mbegu kutoka Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI), Emmanuel Mwakatobe, akiwafunza wadau Magereza, namna ya kuweka dawa kwenye mbegu.

ACP Mbena anafafanua: "Kwa mfano, kama umelima vizuri mbegu ya mpunga, unaweza ukazalisha gunia 40 hadi 45 kwa ekari, lakini wao wanazalisha gunia 15 hadi 20 na mahindi unaweza kuzalisha gunia 30 kwa ekari.

"Lakini sisi tunazalisha gunia 12 had 15 na sasa ili kuondoa hili. Tunavaa silaha twende tukapambane na tuhakikishe mbegu zinakuwa bora na tujue kuwa tunakwama wapi katika uzalishaji. Ni sisi wenyewe au ni mbegu tumtafute mchawi," anasema Mbena

Mdau huyo kutoka Magereza anakiri mafunzo waliyopata kutoka TOSCI yamewasaidia kutambua uhalisia, akitaja sio kila mbegu shambani au inayoanguka inapaswa kupewa sifa ya mbegu.

Anasema wamejifunza kuwa mbegu sahihi na kamili ni inayopitia taratibu maalum za uzalishaji mbegu.

Kamishna Mbena anasema, wao maofisa wanne kutoka Magereza ya Arusha, Simiyu, Bariadi na wawili kutoka Dodoma, wamepata elimu anayoamini itawasaidia kutekeleza azma ya uzalishaji mbegu bora zinazojitosheleza nchini na nje ya nchi, baada ya kusajiliwa na TOSCI.

"Kama jeshi tumedhamiria kutekeleza azma hiyo ya kuwa wazalishaji wakubwa wa mbegu bora na tunaweza, sababu tunao wataalamu wa kutosha nchi nzima waliobobea kwenye Magereza mbalimbali, yakiwemo ya kilimo nchini, tukijumlisha na maofisa waliopata mafunzo tunakuwa tumepiga hatua kubwa," anaeleza.

Mkuu huyo wa Magereza, anasema uzalishaji mbegu hizo utasaidia kupunguza gharama za uendeshaji katika uzalishaji, pale inapoacha kununua mbegu zisizo sahihi kwa wazabuni.

Pia, anasema itawapunguzia gharama za uendeshaji katika uzalishaji bidhaa za shambani na hasa kwenye ununuzi wa pembejeo za kilimo.

Kwa mujibu wa tovuti ya Magereza mkoani Morogoro, aliko ACP Mbena, kuna gereza moja la wilaya, ambalo ni la Mkono wa Mara, kisha matano ya kilimo; Wami Kuu, Mtego wa Simba, G/Wanawake, Wami Vijana na Kihonda na kambi moja la Mkumbo.

**OFISA KILIMO**

Mrakibu Nimuindaeli Mziray kutoka Kitengo cha Kilimo na Mifugo, Magereza Dodoma, anaipongeza TOSCI kuwapata elimu sahihi, anayoamini itaisaidia jeshi kuzalisha mbegu bora zitakazokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

Anasema, kuna matatizo wanayokutana nayo kuhusiana na mbegu zao kutokuwa na ubora na zimekuwa zikikosa mazao ya kutosha, katika miaka ya nyuma na imekuwa ikitokana na kukosa elimu ya kutosha.

Ni katika mazingira yanayofanana na hayo ya elimu, Mrakibu Mziray anaamini italisaidia jeshi kuanzisha maandalizi ya shamba, kupanda, utengano na ukaguzi wa kutoa mazao tangu shambani ambayo hayafanani na mbegu bora.

**MKUFUNZI TOSCI**

Akizungumzia hilo, Mkufunzi wa Mafunzo ya Mbegu Bora kutoka TOSCI, Emmanuel Mwakatobe, anasema wamewapa mafunzo ya uzalishaji mbegu maofisa wa Magereza kwa wiki moja, wakilenga kuwajengea uwezo wa kuzalisha tangu shambani na kimaabara, kwa kuzingatia sheria za mbegu.

Mwakatobe ambaye pia ni Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Ubora wa Mbegu kutoka Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu, anasema amewapa elimu ya kuchakata mbegu baada ya kulimwa shambani, kwa kutumia nguvu za kibinadamu au mashine na kuelekeza shughuli zote za uzalishaji zingatie ubora unaohitajika.

Mkufunzi huyo anasisitiza kutambuliwa umuhimu mbegu na ubora unaotakiwa katika viwango vilivyowekwa, kwa mujibu wa kanuni na sheria za mbegu, kabla haijamfikia mkulima aliko.

Anasema uwekaji dawa kwenye mbegu wakati wa kuhifadhi maghala ni vyema ukafuata sheria na kanuni zilizopo kutokana na baadhi ya wazalishaji kuharibikiwa na mbegu katika hatua hiyo ya mwisho kwa kuzidisha maji, au kuzidisha dawa au kupunguza dawa.



Kamishna Msaidizi Roswin Mbena, wa Jeshi la Magereza **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE.**

## ORODHA YA MAGEREZA NCHINI


| S/NO | MKOA | MAGEREZA MAKUU | MAGEREZA YA WILAYA | MAGEREZA YA KILIMO | KAMBI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ARUSHA | Arusha | | | |
| | | | | Mang'ola | |
| | | | Loliondo | | |
| 2 | DAR ES SALAAM | Ukonga | | | (i) Mvuti (ii) Kimbiji |
| | | Keko | | | |
| | | Segerea | | | |
| | | | | Wazo Hill | |
| 3 | DODOMA | | Kongwa | | Mkoka |
| | | | Kondoa | | |
| | | | Mpwapwa | | |
| | | | | King'ang'a | |
| | | | | Msalato | |
| | | Isanga | | | |
| | | | | | |
| 4 | IRINGA | | Iringa | | (i) Mlolo (ii) Igumbilo |
| | | | | Isupilo | |
| | | | Njombe | | (i) Ihanga (ii) Mdandu (iii) Kidewa |
| | | | Makete | | |
| | | | | Mgagao | |
| | | | | Pawaga | |
| | | | | Ludewa | |
| 5 | KAGERA | | Biharamulo | | Nyarumbungu |
| | | | Bukoba | | |
| | | | | Kitengule | |
| | | | Muleba | | |
| | | | | Rwamrumba | Nkindo |
| | | | Ngara | | |
| | | | Kayanga | | Kihanga |
| | | | | Rusumo | -- — |
| 6 | KIGOMA | | Bangwe | | |
| | | | | Ilagala | Burega |
| | | | Kasulu | | Makere |
| | | | Kibondo | | |
| | | | | Kwitanqa | |
| 7 | KILIMANJARO | Karanga | | | Kifaru |
| | | | Same | | |
| | | | Rombo | | |
| | | | Mwanqa | | Shamba Kigonqoni |
| 8 | LINDI | | | Kingurungundwa | |
| | | | Nachingwea | | |
| | | | Kilwa | | Mtanga |
| | | Mah. Lindi | | | |
| | | | Li wale | | |
| 9 | MANYARA | | Babati | | Magugu |
| | | | Mbulu | | |
| | | | Kiteto | | |
| 10 | MARA | | | Mugumu | |
| | | | | Kiabakari | |
| | | | Mah. Mugumu | | |
| | | | Tarime | | |
| | | | Bunda | | |
| | | | Musoma | | Butiama |
| 11 | MBEYA | | Mbarali | | |
| | | Ruanda | | | Kawetele |
| | | | | Songwe | |
| | | | Tukuyu | | Kyela |
| | | | | Ngwala | Mkwajuni |
| | | | Ileje | | |
| | | | Mbozi | | |
| 12 | MOROGORO | | | Mkono wa Mara | |
| | | | | Wami Kuu | |
| | | | | Mtego wa Simba | Mkumbo |
| | | | | G/Wanawake | |
| | | | | Wami Vijana | |
| | | | | | |
| | | | | Kihonda | |
| | | | Kilosa | | |
| | | | Mahenge | | |
| | | | Mah. Morogoro | | |
| | | | | Mbigili | |
| | | | | Idete | |
| | | | | Kiberege | |
| 13 | MTWARA | Lilungu | | | |
| | | | Newala | | |
| | | | Masasi | | |
| | | | | Chumvi | |
| | | | | Namajani | |
| 14 | MWANZA | Butimba | | | |
| | | | Geita | | |
| | | | Ukerewe | | Bugorola |
| | | | Ngudu | | Malya |
| | | | Magu | | |
| | | | | Kasungamile | Sengerema |
| | | | | Butundwe | |
| 15 | PWANI | | | Kigongoni | Kimara |
| | | | Utete. | | |
| | | | Mafia | | |
| | | | Mkuza | | |
| | | | | Kibiti | Kopea |
| | | | | Kilombero | |
| | | | | Ubena | Mgogodo |
| 16 | RUVUMA | | | Kitai | |
| | | | | Mkwaya | |
| | | | Mah. Songea | | |
| | | | Tunduru | | |
| | | | | Majimaji | |
| | | | Mbinga mjini | | |
| 17 | RUKWA | | | Kulilankulunkulu | |
| | | | | Molo | |
| | | | Mpanda | | |
| | | | M/Sumbawanga | | |
| | | | Kitete | | |
| 18 | SINGIDA | | Manyoni | | Chikuyu |
| | | | Singida | | Singa |
| | | | Kiomboi | | |
| | | | | Ushora | Uganda |
| 19 | SHINYANGA | | Shinyanga | | Ning'hwa |
| | | | Maswa | | |
| | | | Malya | | |
| | | | Kahama | | |
| | | | Bariadi | | |
| | | | | Kanegele | |
| | | | | Matongo | |
| | | | Meatu | | |
| 20 | TABORA | Uyui | | | Kazima Kasisi |
| | | | Mah. Tabora | | |
| | | | Nzega | | |
| | | | Mah.Urambo | | |
| | | | Igunga | | |
| | | | | K/Urambo | |
| 21 | TANG A | Maweni | | | Mgwisha |
| | | | Pangani | | Mivumoni 'C' |
| | | | Lushoto | | Yoghoi |
| | | | Mah. Tanga | | Kilulu |
| | | | Handeni | | Kwabaya |
| | | | | Kwamngumi | |
| | | | | Mng'aro | |
| | | | Korogwe | | Komsala |
| | **Jumla** | 12 | 68 | 46 | **40** |

!

- Jedwali kutoka Tovuti ya Jeshi la Magereza.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Ni ushauri tu kwa Rais JPM






**NA JOSEPH KULANGWA**

KAMA kuna kitu alikiahidi kwa dhati kabisa wakati anazindua Bunge la 11 Novemba 2015, Rais Dk. John Magufuli, mara tu baada ya kuingia madarakani, ni kile cha kubana matumizi serikalini.

Hicho hata mtu utoke kwenu uje kwetu umelewa chakari, lazima utakishuhudia, tena hutahitaji elimu ya darasani na wala maji ya kunywa au supu kutambua.

Rais JPM alikataa kabisa kusafiri safari nje ya nchi pamoja na wasaidizi wake wa karibu. Na kama kulikuwa na ulazima, sharti ni maombi ya kibali maalumu.

Aliweza na hakutoka kukanyaga si Ulaya, Asia, wala Marekani, alicheza hapa hapa Afrika na tena si nchi nyingi. Yeye alisema watakuja tu na huko walikoma, balozi wetu watayajenga tu. Acha fedha zetu badala ya kutumika kwa nauli na miposho,tujenge mambo ndani ya nchi.

Nani mlemavu kwa kuona katika haya? Nani hajaona? Yaani ushindwe kusoma maandishi kweli hata picha huzioni? Acheni hizo bhana. Siko hapa kuorodhesha aliyoyafanya kwa sababu mtakinahi bure, kwani ni sawa na kulishwa mpaka ukavimbiwa na kuongezwa, utakinahi. Jioneeni wenyewe.

Hivi sasa pamoja na kwamba naye kishatia nia ya kurudia angalau kwa miaka mingine mitano, ni muda mwafaka naye kutafakari juu ya aliowapa dhamana kumsaidia, kama waliweza au hawakuweza, ingawa alikuwa akiwashughulikia pale pale waliochezea wembe.

Aliwaaminisha na vijana, wapo waliomsaidia lakini wapo waliomwangusha. Aliwaamini pia wazee, wapo waliomsaidia na wapo waliomwangusha. Lakini, nao wajitafakari wasijemlaumu wasiporejea, huku wakijua Watanzania tunakaribia idadi ya milioni 60. Kwani na si hatutaki kumsaidia? Waone!

Mimi leo, kwa kuwa naamini atarudi kama ilivyo ada kwa Watanzania, kwa mujibu wa ka-utaratibu ketu ka miaka kumi kumi, nataka kushauri tu kama itampendeza akija tena afanye hivi.

Huku akiendelea kubana matumizi hivi hivi lakini, ili miradi ikamilike na Tanzania ya Viwanda hatimaye tuishi, natembea kwenye maneno ya aliyekuwa Spika wa Bunge la 11, Job Ndugai, ambaye alisema kitu fulani nadhani akikiona kidogo, lakini mimi nikakiona kikuubwa!

"Unakwenda mahali unakuta bango la kuonyesha shule lina maneno meengi mpaka kusoma kulimaliza karibu dakika ngapi sijui

"Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Halmashauri ya Wilaya ya Musoma Mjini. Shule ya Msingi…. Sanduku la Posta 1234. Musoma, Mara…'"

Sasa utakuta zingine mpaka zimeandikwa 'Motto' ya Shule. Sijui ni kitu gani hicho, pengine ni kaulimbiu ya shule. Zingine utakuta mpaka sheria za shule nazo zipo hapo!

Nilimpongeza Ndugai kwenye ile sekondari iliyojengwa na wabunge na wadau wao Dodoma, jina halina madoido hayo. Bali 'Sekondari ya Wasichana Bunge'. Kwishney. Safi sana.

Sasa hiyo inatakiwa pia iende kwenye majina ya wizara. Hapa sasa ndio ushauri wangu kwa JPM. Mathalan, kwa nini kuwa na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Watoto, Wanawake na Wazee! Ndefu sana hiyo.

Nashauri iwe hivi: Ofisi ya Rais Utawala Bora; Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano; Ofisi ya Waziri Mkuu, Makazi na Mitaa; Wizara ziwe ifuatavyo: Ya Ulinzi; ya Usalama na Uhamiaji ikiwa na Naibu Waziri; Afya na Naibu; Elimu na Utumishi na Naibu; Sheria na Kazi na Naibu; Biashara na Viwanda na Naibu; Kilimo na Mifugo na Naibu; Maji na Uvuvi na Naibu; Ardhi na Madini na Naibu; Hifadhi na Utalii; Nishati na Naibu; Usafirishaji na Miundombinu na Naibu; Mambo ya Nje na Naibu; Habari na Mawasiliano na Naibu na Utamaduni na Michezo.

Kinachonifikisha hapa, ni kuona kwa nini TAMISEMI inaingiliana na Afya na Elimu. Kwanini mambo ya habari yasiwe pamoja na mawasiliano, kwani mara nyingi vyombo vya habari vimekuwa vikihusishwa na mawasiliano.

Kwanini anayeshughulikia mji asishughulike pia na yaliyomo majini? Kwa nini wafuga jina wakulima watenganishwe wizara tofauti? Pia, watumishi wanatokana na elimu. Afya ni mtambuka kila binadamu anaingia huko.

Makazi yako mitaani. Nje ni pamoja na Afrika Mashariki. Madini yako ardhini. Usafirishaji unategemea miundombinu, utamaduni na michezo ni pacha na Katiba ndiyo sheria kuu. Alamsiki.

**• Simu: +255 713 410008 na barua pepe:jkulangwa@yahoo.com**

UCHUMI

MAHARI NG'OMBE SHIDA!

# DC anusuru mwanafunzi miaka 13 kuolewa, tatizo sugu Kwimba

## • Baba: Ninao 14, huyu wa 13...sirudii
## • Walimu, maofisa kata walia na tabia

**Na Neema Emmanuel, KWIMBA**

JANA ilikuwa na sehemu kwanza ya mfululizo wa makala hizi, ikuhusu kukithiri tabia ya mimba na ngono kwa wanafunzi wa kike. Lakini kwanini tabia hii? Kunaonekana kuwepo tatizo, zaidi ya ufafanuzi ngazi ya tabia binafsi. Wazi nao wana nafasi yao. Kwa vipi?

Ndani ya jamii za Ukanda wa Ziwa, rasilimali ng'ombe ni uchumi mkuu, ikizingatiwa asili ya maisha ya kifugaji. Hata thamani ya ndoa inadhihirishwa kwa ulinganifu wa idadi ya ng'ombe wanaotolewa.

Ni katika mtazamo huo, wako watoto walioingia katika michakato hiyo katika mvuto wa mabadilishano ya mahari ng'ombe na mabinti ambao umri bado ni stahili wako masomoni.



Ofisa Tarafa ya Ibindo, Jeremiah John.

Ndicho kilichotokea, pale Mkuu wa Wilaya ya Kwimba, Senyi Ngaga, alipomnusuru binti Pili (siyo jina lake halisi) katika umri wa miaka 13. Sasa anasoma kidato cha pili katika shule ya sekondari wilayani hapa.

Mkasa ulivyo, baba mzazi aliafikiana na 'mchumba' kwa mabadilishano ya ng'ombe. Nusura hiyo, ni tukio lililoota sura mpya kwa maisha ya binti kuondolewa vikwazo, dhidi ya malengo yake, ikiwamo kiafya.

Mkuu wa Wilaya ya Kwimba, Senyi Ngaga, anaisimulia Nipashe, kwamba Pili alikumbwa na mkasa huo baada ya baba yake kumuingiza katika mchakato wa ndoa.

Anasema, alipopata fununu za kuozeshwa binti huyo kinyume na sheria, aliingilia kati kuwakamata wazazi, kitu kilichonusuru mtoto na hadi sasa anaendelea na masomo.

Senyi anasema ni changamoto anayokumbwa nayo kwa jamii ya Kwimba kupenda kumiliki ng'ombe, hivyo, ikawafanya watoto wa kike kuwa chanzo cha utajiri au mali katika familia.

**MZAZI/WADAU**

Nipashe ilipomdadisi baba mzazi wa binti, Nyamasele Nyanda, anakiri tukio hilo, akiweka wazi ana jumla ya watoto 14 na anayetaka kumuozesha ni wa 13.

Kuhusu suala la kuendelea kumuozesha, anakiri hatoendelea nalo na sasa amejikita katika kumpatia binti hiyo elimu, akifafanua: "Nikimuozesha mtanikamata kwa sasa nimemuacha asome hadi pale atakapoishia yeye mwenyewe.

"Sasa yupo kidato cha pili, siwezi kabisa kumuozesha akiwa anasoma, lakini akishindwa ataolewa, akifaulu ataendelea na masomo yake, sasa kazi kwake kusoma kwa nguvu zote."

> **"Hivi karibuni kuna binti alifaulu kuingia kidato cha kwanza, lakini tayari baba yake alikuwa kishachukua mahari na hivyo tuliingilia kati," anasimulia na kuongeza:**



Baba wa mtoto aliyenusurika kuolewa, Nyamasele Nyanda .

Anasema, ameshapewa funzo na Mkuu wa Wilaya na aache ubaguzi kwa watoto kwa kuwapa mahitaji sawa, bila kujali jinsia na Mzee Nyanda akisema: "Mwanangu anaenda shule vizuri siyo mtoro, mimi mwenyewe baba yake nipo lazima atasoma tu."

Mwalimu wa binti huyo, ambaye hakupenda kutajwa jina, anasimulia: "Binti anaendelea vizuri na masomo na hata leo alikuwa hapa kuchukua maswali ya kufanya nyumbani (Siku tatu kabla shule kufunguliwa)."

Mwalimu huyo anafafanua kuna walakini katika jamii, wanapenda kupewa ngo'mbe kwa mbadala wa binti na baada ya kufanikisha hilo, huwa kuna visingizio vingi vinavyohusiana na masomo ya binti husika, lengo kufanikisha azma yao.

Baba wa mtoto aliyenusurika kuolewa, Nyamasele Nyanda .



Mkuu wa Wilaya ya Kwimba, Senyi Ngaga akizungumza. **PICHA ZOTE: NEEMA EMMANUEL.**

Anakumbusha, mazingira ya mabinti kukaa nyumbani hatari na jambo jema ni ujenzi wa mabweni, yanayosaidia kuwaweka salama.

John Buluhya, Mchungaji wa Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT) Nyambiti, anaitaka jamii jirani ibadilike na kutenda mema, kwani yanayotokea yanarudisha nyuma maendeleo yao na nchi kwa ujumla, kumuoza mtoto mdogo, tena katika mazingira yaliyokosa ridhaa.

**MAOFISA SERIKALI**

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nyambiti, Mongo Mbombile, anasema matukio ya kuwaozesha watoto huko ni mengi akiwalaumu wazazi wanaopenda thamani ya mifugo kuliko elimu, kwa maisha ya baadaye ya mtoto.

"Wazazi sasa wana mbinu mpya ya kuomba uhamisho. Usifikirie kuwa ukimpa mtoto ataenda kusoma, hapana hiyo ni tiketi ya kwenda kumuoza. Hivi sasa kuna 'ka-utaratibu kapya' kwa watoto wanaohamishwa wengi wakielekea Mpanda hasa wa kike," anasema Mombile.

Jeremiah John, Ofisa Tarafa ya Ibindo, anasema tatizo wazazi wengi hawajui umuhimu wa elimu kwa mtoto, hivyo jukumu lao ni kuwakamata wazazi, ndugu na marafiki watakaohudhuria hafla ya utoaji mahari ya mwanafunzi na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

"Hivi karibuni kuna binti alifaulu kuingia kidato cha kwanza, lakini tayari baba yake alikuwa kishachukua mahari na hivyo tuliingilia kati," anasimulia na kuongeza:

"Hata, hivyo kuna mtoto mwingine wazazi wake walikuwa wanapokea mahari, kilichofanyika ni kuwakamata watu wote waliokuwa eneo la tukio, jambo lililosaidia matukio kupungua."

John anasema, kwa kushirikiana na ngazi mbalimbali za wilaya, ikiwamo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na vyombo vya usalama, walifuatilia sana, hata imesaidia kujenga hofu kwa jamii kuanza kuachana matendo hayo.

• ***Soma mikasa zaidi Alhamisi ijayo.***



# TANESCO yashauri ukarabati vifaa viwandani

**Na Mwandishi Wetu,**

DODOMA

SHIRIKA la Umeme (TANESCO), limewataka wamiliki wa viwanda kufanya ukarabati wa mara kwa mara wa vifaa vilivyotumika kwa muda mrefu, ili kuondokana na matumizi makubwa ya umeme.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mhandisi Mtafiti wa Shirika hilo, Aurea Bigirwamungu, alipokuwa akitoa elimu ya matumizi bora ya nishati ya umeme katika Wilaya za Bahi na Dodoma.

Alisema wamiliki hao wanatakiwa kuwa na utamaduni wa kufanya ukarabati huo ili kujiepusha na gharama zisizo za lazima na matumizi hayo makubwa.

"Wamiliki wanatakiwa kuwa na utamaduni wa kubadilisha mota za kuendeshea mitambo yao katika uzalishaji ili kutumia nishati ya umeme inayoendana na gharama ya matumizi sahihi ya nishati ya umeme kwenye viwanda vyao," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Tawala wa Kampuni ya Nyanza Road Workers, Bakari Mugini, alishukuru kwa kupatiwa elimu hiyo ambayo imesaidia kujua matumizi ya umeme kwa kampuni.

"Tumepata elimu juu ya usalama wa miundombinu iliyopo viwandani ili kuongeza uzalishaji katika kampuni zao," alisema.

Alisema elimu iliyotolewa na shirika hilo itasaidia kutoa huduma bora kwa wananchi na kuhakikisha umeme mkoani Dodoma unakuwa wa uhakika.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akisaini kitabu cha maombolezo ya kifo cha Balozi Job Lusinde nyumbani kwa marehemu Kilimani, jijini Dodoma juzi. Balozi Lusinde alifariki dunia Julai 7 mwaka huu, jijini Dar es Salaam na anatarajiwa kuzikwa leo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yazipongeza PLAJC, TGNP kuelekea uchaguzi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imeipongeza Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Kituo cha Amani Haki na Msaada wa Kisheria Tanzania (PLAJC), pamoja Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kuimarisha ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika uchaguzi mkuu 2020.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tixon Nzunda, wakati wa kikao cha mashauriano na mkakati wa kuwa na uchaguzi jumuishi na wa amani wenye ushirikishwaji mkubwa wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kama sehemu kubwa ya jamii, watumie fursa iliyopo kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi Mkuu 2020.

Alitaka vyama vya siasa viimarishe mifumo yao ya ndani ya namna ya kuwapata viongozi katika njia za kidemokrasia na kutoa usawa kwa makundi yote ya kijamii kwa kuzingatia katiba na sheria za nchi.

Pia, aliwataka wananchi kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi Mkuu kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi ili kuitumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi kwa kujitokeza kwa wingi.

"Tudumishe utulivu, amani, mshikamano pamoja na ustaarabu wetu wa Kitanzania katika kipindi chote cha kampeni na uchaguzi mkuu ili kulifanya taifa letu kuendelea kuwa kisiwa cha amani na mfano wa kuigwa barani Afrika na duniani kwa ujumla," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema uchaguzi wa mwaka huu unawapa matumaini makubwa kwamba wanawake, vijana na wenye ualemavu watajitokeza kwa wingi.

Alisema hali hiyo itasaidia kuiweka Tanzania, katika nafasi nzuri ya utekelezaji wa mikataba ya kikanda na kimataifa juu ya usawa wa kijinsia na maendeleo.

Mkurugenzi wa PLAJC, Jaruo Karebe, alisema kikao hiko ni cha mashauriano na mikakati ya kuhakikisha mazingira wezeshi na kuimarisha ushiriki wa wanawake, vijana na wenye ulemavu katika mchakato mzima wa uchaguzi.

Alisema, kikao hicho kiliwakutanisha wadau mbalimbali wa demokrasia na uchaguzi, viongozi wa serikali, viongozi wa dini na asasi za kiraia, na kililenga kuja na mkakati wa pamoja wa namna ya kutatua changamoto za ushiriki wa makundi hayo.

# TPSF yaomba sera kuendeleza sekta binafsi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Sekta Binafsi Mkoa wa Dodoma (TPSF), imeshauri serikali kuifanyia kazi na kupitisha sera ya kutambua na kuendeleza sekta binafsi nchini ili kukuza zaidi uchumi wa Taifa.

Hayo yalielezwa jana na Mwakilishi wa Taasisi ya Sekta Binafsi Mkoa wa Dodoma, Ringo Iringo, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, jijini hapa.

Alisema sekta binafsi wanaipongeza serikali katika jitihada zake za kulisaidia Taifa kuingia katika orodha ya nchi zenye uchumi wa kipato cha kati duniani.

Alisema pamoja na taifa kuingia katika hatua hiyo, bado ipo haja kwa serikali kuhakikisha kuwa sera ya kutambua sekta binafsi inaletwa bungeni na kupitishwa ili iongeze kasi ya ukuaji wa uchumi.

"Bado hakuna sera wala sheria ya kutambua kuwa sekta binafsi ni moja ya muhimili, katika ukuaji wa uchumi kwenye taifa, hivyo tunaiomba serikali kuleta sera hii ya kutambua na kuendeleza sekta binafsi ili kusaidia ukuaji wa uchumi katika taifa letu," alisema Ringo.

Pia alisema sera hiyo itasaidia kuwezesha sekta binafsi, kupiga hatua kutokana na kuhakikisha kwa kupata mikopo ya muda mrefu kutoka taasisi za kifedha.

Kadhalika alisema, kupata mikopo katika taasisi za fedha nchini kutasaidia kuongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ambazo zitasafirishwa nje ya nchi na kusaidia kupata fedha za kigeni.

"Wenzetu Kenya, walishaingia katika uchumi wa kati muda mrefu ndio maana unaona hivi sasa wanasafirisha sana kuliko sisi ni kutokana pia na kupata fursa ya mikopo 'access to finance' na hii ni mikopo ya kimaendeleo ambayo na sisi tutaanza kuipata kutokana na kuingia katika uchumi wa kati," alisema.

Vile vile, alizitaka taasisi za kifedha nchini kubadilisha mitazamo katika utoaji wa mikopo na kuanza kuwezesha kifedha sekta ya kilimo, mifugo na utalii.

"Sekta hizi zitasaidia kukuza uchumi wa taifa, kwani katika kilimo ndiko tunaweza kupata malighafi ambazo zitasaidia kuzalisha bidhaa bora, na kusafirisha nje na kupata fedha za kigeni, lakini pia utalii pamoja na mifugo ni sehemu nyingine itakayo kuwa msaada kwetu katika sekta binafsi kuleta wawekezaji nchini," alisema Ringo.





# Mwakagenda ajitosa CHADEMA Rungwe

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MTIFUANO wa kuwania ubunge Jimbo la Rungwe, umepamba moto ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), baada ya wanachama saba kujitokeza kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya kukiwakilisha chama hicho kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi alipokuwa anamkabidhi fomu za kuomba uteuzi, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya kupitia chama hicho, Sophia Mwakagenda, Katibu wa CHADEMA Jimbo la Rungwe, Award Kalonga, alisema lengo la chama hicho ni kulikomboa jimbo hilo kutoka CCM.

Kalonga alisema kati ya wanachama hao saba, mwanamke ni mmoja ambaye ni Mwakagenda, na kwamba historia ya jimbo hilo inaonyesha halijawahi kuongozwa na mwanamke, lakini endapo mama huyo atashinda kwenye kura za maoni, chama kitahakikisha anashinda.

Alisema baada ya chama hicho kugaragazwa na CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, kiliendelea kuwapima wanachama wake kwa ajili ya kuangalia wenye sifa na kwamba mpaka sasa waliojitokeza wana sifa za kukiwezesha chama kushinda.

"Lengo la chama chetu ni kulikomboa hili jimbo, sasa tunawaeleza watia nia wetu kwamba yeyote atakayeshinda kwenye kura za maoni, lazima wote tumuunge mkono na kumuuza kwa wananchi mpaka tushinde," alisema Kalonga.

Katibu Mwenezi wa CHADEMA Wilaya ya Rungwe, Juma Mwambelo, alisema chama hicho kitapata ushindi kwa maelezo kuwa kina mbinu za kupata wagombea wenye sifa.

Alisema mgombea anayetakiwa na chama hicho ni yule ambaye anafahamika kuwa anaomba nafasi hiyo kwa ajili ya kwenda kutetea maslahi ya wananchi na sio wale ambao wanapambania maslahi yao binafsi.

Alisema kwa sasa chama hicho kinafanya kazi vizuri na mamlaka mbalimbali za serikali likiwamo Jeshi la Polisi pamoja na viongozi wengine wa serikali, hivyo wana uhakika wa kutohujumiwa kwa namna yoyote.

"Sisi kama chama tunampongeza sana mama Mwakagenda kwa kujitokeza katikati ya wanaume saba, huu ni uthubutu wa hali ya juu, lakini pamoja na yeye ni kwamba wagombea wetu wote wako vizuri na wanauzika kwa wananchi," alisema Mwambelo.

Kwa upande wake Mwakagenda, alisema endapo atashinda kwenye kura za maoni, atahakikisha anawaunganisha wananchi wa Rungwe bila kujali tofauti ya itikadi zao za kisiasa ili kuleta maendeleo kwenye sekta mbalimbali.

Alisema katika wilaya hiyo kuna fursa mbalimbali ambazo wananchi hasa vijana wanatakiwa waunganishwe nazo kwa ajili ya kujiajiri, na kujiletea maendeleo wao wenyewe na taifa.

Alisema moja ya fursa hizo ni biashara ya mazao mbalimbali yakiwamo mahindi, kakao, viazi na ndizi ambazo kwa sasa fursa hizo zinachangamkiwa na wageni kutokana na wenyeji kukosa mitaji. "Tutawaunganisha vijana kwenye vikundi na kuwakopesha asilimia yao nne ya mapato ya ndani ya halmashauri ili wanunuwe mazao wapeleke Dar es Salaam wakauze badala ya watu kutoka huko kufuata mazao yetu huku," alisema Mwakagenda.

Vilevile, alisema endapo atachaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hilo atahakikisha anapambana kwa ajili ya kuboresha kilimo cha chai, kakao, kahawa na maparachichi ambayo yana soko kubwa duniani kwa sasa.




Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya kwa tiketi ya CHADEMA, Sophia Mwakagenda (wa pili kushoto), akipokea fomu kutoka kwa Katibu wa CHADEMA Jimbo la Rungwe, Award Kalongya, juzi, kwa ajili ya kugombea ubunge wa Jimbo la Rungwe. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Nyanda za Juu waonyeshwa fursa za kilimo cha mazao lishe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameshauriwa kuchangamkia kilimo cha mazao lishe ambayo yamefanyiwa utafiti.

Mazao hayo yamefanyiwa utafiti na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya ambayo ni kwa ajili ya chakula na biashara.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema wamezalisha mbegu za kutosha za mazao lishe ambayo ni mahindi, maharage na viazi ambayo yana virutubisho vya kutosha kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto.

Alisema mazao hayo yanastawi vizuri katika mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, ambayo kiwango cha udumavu kwa watoto kipo juu kuliko hata maeneo ambayo hayazalishi chakula kwa wingi.

"Mazao haya yana soko kubwa sana, lakini mbali na kuwa na soko pia yanatumika kwa ajili ya chakula, na yana vitamini ambazo ni muhimu kwa ajili ya kukabiliana na udumavu kwa watoto, tusisubiri watoto wapate shida ndio tuanze kutafuta dawa," alisema Dk. Bucheyeki.

Aliwataka wananchi wanaohitaji kulima mazao hayo kwenda kwenye taasisi hiyo ili wapate mbegu na wakapande kwenye maeneo yao na kwamba watapewa elimu ya kilimo cha kisasa cha mazao hayo.

Dk. Bucheyeki pia alisema wameandaa mashamba darasa kwenye mashamba ya taasisi hiyo ambayo wanayatumia kufundishia wakulima kilimo cha kisasa, na chenye tija hivyo kila anayehitaji elimu hiyo anafundishwa kwa vitendo.

# Mkurugenzi Jiji ahimiza ushirikiano wa watumishi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKURUGENZI Mtendaji wa Jiji la Mbeya, Elias Amede, amewataka watumishi wa halmashauri hiyo kuendeleza ushirikiano waliokuwa wanampatia wakati akiwa mwekahazina wa jiji hilo, ili kuendeleza mikakati waliyojiwekea ikiwamo ukusanyaji wa mapato.

Alitoa ushauri huo alipofanya kikao cha kwanza na watumishi hao tangu alipoteuliwa na Rais John Magufuli, ambapo aliwataka watumishi wote kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii na kwa ushirikiano ili kufikia malengo ya maendeleo.

Alisema yeye ni muumini wa kuzingatia muda katika kila jukumu analotekeleza, hivyo ni vema kila mtumishi ajifunze kuzingatia muda wa kuingia kazini na kutekeleza majukumu kwa ufasaha.

"Mimi ni yuleyule ambaye tulikuwa tunafanya kazi wote nikiwa mwekahazina wa Jiji hili, lakini kilichobadilika ni cheo tu, hivyo naomba tuzingatie yale yote ambayo tulikuwa tumekubaliana tangu awali, tuhakikishe tunatekeleza majukumu yetu kwa ushirikiano," alisema Amede.

Aliwataka watumishi kila mmoja kuwasilisha taarifa za utendaji kazi wake ili wajipime kama utendaji kazi wao unapanda ama unashuka na wajue madhara ya kila wanachokosea.

Vilevile, alisisitiza usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya halmashauri hiyo pamoja na kusimamia matumizi ya fedha zinazokusanywa ili kuliwezesha Jiji kuendelea kupata hatisafi, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alimpongeza Amede kwa utendaji kazi wake mzuri, ambao ulimwezesha kuonekana na kuaminiwa na Rais Magufuli.

Aliwataka watumishi kuendelea kujituma na kuiga mfano wa Amede pamoja na aliyekuwa Ofisa Mipango wa Jiji hilo, Saad Mtambule, ambaye aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Ntinika alisema Jiji la Mbeya lina matatizo mbalimbali ambayo yanatakiwa kutatuliwa kwa ushirikiano wa hali ya juu, na kwamba wasije wakawa wanamdharau Amede kwa sababu walikuwa wanafanya naye kazi kwenye ofisi moja.

"Hata mimi kwenye utumishi wangu nilianzia ngazi za chini kabisa na baadaye niliteuliwa kuwa mkurugenzi na sasa ni Mkuu wa Wilaya, hivyo kila mmoja ajitume kwenye majukumu yake ili kufikia mafanikio ambayo hawa wenzetu wameyapata," alisema Ntinika.

Alipokuwa anawaapisha wakuu wa mikoa na kushuhudia viapo vya maadili ya utumishi wa umma vya wakuu wa wilaya na wakurugenzi aliowateua hivi karibuni, Rais Magufuli alisema aliwateua watumishi wawili wa Jiji la Mbeya kuwa wakurugenzi kwa sababu walifanya kazi kubwa kwenye ukusanyaji wa mapato na kufikia asilimia 103.



Mfugaji wa kuku, Bahati Issa mkazi wa Kijiji cha Kikungwi, Kusini Unguja akiihudumia mifugo yake jana. Ufugaji wa kuku ni moja ya nyenzo ya kuwakomboa wanawake kiuchumi visiwani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Asasi yaonya rushwa katika uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIONGOZI na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wametakiwa kuepuka kutoa na kupokea rushwa katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Ofisa Elimu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), Yussuf Juma, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na viongozi wa matawi, wadi na majimbo ya Mkoa wa Mjini kichama katika kikao kilichofanyika ukumbi wa CCM, Amani. Alisema kitendo cha kupokea na kutoa rushwa katika chama kinasababisha kutompata mgombea mwenye uwezo wa kuwatumikia wananchi.

Yussuf alisema dhamira ya uchaguzi ni kupatikana kiongozi atakayetekeleza ilani ya chama katika kuwapelekea maendeleo wananchi. Alisema uchaguzi bila ya rushwa inawezekana, hivyo aliwaomba viongozi hao kuendelea kuwa wazalendo kwa kukataa kuchukua au kutoa rushwa.

Naye Ofisa Elimu wa Mamlaka hiyo, Saada Salum Issa, alisema ZAECA inaendelea kupokea taarifa zinazohusu rushwa, hivyo akawataka viongozi wa vyama vyote vya siasa kutoa ushirikiano endapo kutakuwa na viashiria vya masuala ya rushwa.

"Sote kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha tatizo la rushwa linaondoka nchini kwa kutoa taarifa za viashiria vya uwepo wa rushwa ili kutengeneza serikali iliyo sahihi na kuweza kupeleka maendeleo ya wananchi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Marina Joel Thomas, aliwataka wajumbe hao kuachana na tabia hiyo na badala yake wafanye kazi kwa uzalendo.

# Matatani tuhuma kubambwa dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MTU mmoja anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa tuhuma za kukamatwa na dawa za kulevya.

Kamanda wa Polisi Kaskazini Unguja, Kamishna Msaidizi Haji Abdalla Haji, amethibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo.

Alimtaja mtuhumiwa kuwa ni Makame Haji Khamis (34) mkazi wa Nungwi Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja aliyekamatwa na kete 288 zenye uzito wa gramu 6.336 aina ya heroine.

Tukio hilo, alisema lilitokea Julai 7, mwaka huu, saa 4:30 asubuhi huko Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Kwa mujibu wa Kamanda Haji, mtuhumiwa alikamatwa kutokana na jeshi hilo, ikiwa ni mwendelezo wa operesheni za kupambana na wasambazaji, wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevya.

Alisema siku hiyo mtuhumiwa alipatikana na dawa hizo ambazo alizitia ndani ya paketi ya sigara na kuzihifadhi ndani ya mfuko wake wa suruali aliyokuwa ameivaa. Kutokana na kuota mizizi kwa biashara hiyo, Haji aliwataka vijana kutojihusisha na dawa za kulevya na kuwataka watafute kazi zingine za kufanya.

Kamanda Haji alisema mtuhumiwa huyo atapelekwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Wakati huo huo, alisema Jeshi la Polisi mkoa huo lilifanya ukaguzi kwa madereva wanaoendesha vyombo vya moto kinyume na sheria na kubaini makosa 28 na kuwachukulia wahusika hatua mbalimbali.

# Ujenzi hoteli wabadili sura

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema kukamilika kwa ujenzi wa Hoteli ya Mkoani Pemba kutabadilisha mazingira ya wilaya hiyo na kuwa kivutio cha wageni kama zilivyo wilaya zingine.

Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa, aliyaeleza hayo juzi wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa hoteli hiyo.

"Sasa hali iliyofikiwa haitoshi tena kubakia kama ilivyokuwa zamani, ndiyo maana serikali ikatoa uamuzi mzuri hoteli ya Wete kupewa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), hoteli ya Mkoani kupewa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kuifanyia matengenezo na zimebadilisha mazingira na sote tunaona," alisema.

Alisema sasa hoteli ina vyumba 18 vya kulala wageni na itasaidia kuongeza mapato ya serikali.

Hata hivyo, alipendekeza hoteli hiyo na ukumbi wa Umoja ni Nguvu, kufunguliwa kabla ya serikali ya awamu ya saba haijaondoka madarakani.

Alisema wakati umefika kwa miradi ya ZSSF kuwa ya maendeleo itakayokuwa na tija kwa nchi na wanachama.

Pia Balozi Ramia aliutaka uongozi wa ZSSF kuhakikisha hoteli hiyo inaendeshwa kibiashara na si kutoa huduma, kwa kuwa wanategemea kukusanya kodi kisheria, hivyo lazima wageni walipe watakaohitaji huduma hotelini hapo.

Kuhusu mikakati ya ujenzi wa kiwanda cha mwani Chamanangwe, Balozi Ramia alisema serikali imedhamiria zao la mwani na karafuu kufanywa kuwa mazao makubwa ya nchi.

Alisema katika kutilia mkazo hilo, serikali imepandisha bei zao la mwani kutoka Sh. 600 hadi 1,800 kwa kilo huku karafuu bei ikiendelea kama ilivyo sasa.

Kwa upande wa jengo la ofisi za ZRB Pemba, Balozi Ramia alisema azma ya serikali kila ofisi kuwa na majengo ya kisasa ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Joseph Abdalla Meza, alisema mikakati kwa sasa ni kujenga ofisi kila mkoa ili kuwaondolea usumbufu walipakodi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa ina ghorofa moja, ina godown ina fremu 10 na ina eneo kubwa wazi, ipo Dar es Salaam. Mawasiliano 0757 079057


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIUS JOHN KOMBA** anatangaza kupotelewa na cheti cha Ualimu Grade **III** A chenye namba **6578** kilichotolewa na CHUO CHA UALIMU TUKUYU – TTC mwaka 2003. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PWA/BAG/RB/438861/2020.**

115804102

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 65/2020**

**Ombi la GEORGINA NDUKA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu SAMSON MATHAYO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 22/07/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 08/07/2020.

115806102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA**

**SHAURI LA MADAI NA 364 LA 2019**

**TABITHA LUBORA**
**A.K.A MARIAM CHARLES NGESE.................................... MDAI**

**Versus**

1. **FREDRICK SIMON TOWO**
2. **AISHA JUMA.........................................WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: 1. FREDRICK SIMON TOWO**
**2. AISHA JUMA.**

Mnafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ ombi dhidi yenu katika baraza la ardhi na nyumba mkoa wa mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 17/07/2020 katika chumba cha baraza, barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakamama kuu ya biashara, Tanzania. Kwa hivyo mnatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo ninyi wenyewe, wakili wako/ wenu au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria. KAA- Mkijua kwamba kushindwa kufika baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila ninyi kuwepo.
Imetolewa nami kwa amri na chapa ya baraza leo tarehe 01/07/2020.

PHILIP D.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

115806302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA:56..2020**

**Mdai: DANFORD SAMWEL MATESO**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: VERONICA G.NEDEKI**

**Kwa: VERONICA G.NEDEKI**

**Ombi la Mdai: DANFORD SAMWEL MATESO**

**Madai ya: TARAKA,MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO WAWIL I(2).**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 14 mwezi 07 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 09 mwezi 07 mwaka 2020.

115804502

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FOMU II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 73/2020**

**Ombi la RASHIDI MOHAMEDI kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu MONICA AUGUSTINO MJENGI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 22/07/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 09/07/2020.

Sahihi ya Hakimu

115804902

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**Ramadhani Ally Abdallah** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato nne chenye index namba **S.3424-0006** kilichotolewa na Baraza la Mithihani mwaka 2014 katika shule ya sekondari Chongoleni na cheti chenye index namba **P.1430-0074** kilichotolewa na Baraza la Mithihani mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Kiuma. Yeyote atakaviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/KIG/63642/2019.**

115804302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi NA.71/2020**

**Ombi la 1. MARIAM JACKSON NYAU**
**2. OMARI RAJABU kuteuliwa**

**Msimamizi wa mirathi marehemu MWANAHAMIS OMARI RIZIKI**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 10/8/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 8/7/2020

Sahihi ya Hakimu

115806702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 59/2020**

**Ombi la KABURU MWISHEHE kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu MWISHEHE SOGORA MZEE**
**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 13/7/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 13/7/2020

115806602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI WILAYA YA DODOMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**SHAURI LA MADAI 200 na 206 YA 2020**

**MDAI...................................DODOMA PESA LTD**

**DHIDI YA**

**WADAIWA........... 1. ZENA S. HAMISI,**
**2. ELIZABETH CHIMULI**

Kwa kuwa mdai mtajwa hapo juu alifungua mashauri didhi yenu wadaiwa watajwa hapo juu. Mnaarifiwa na Jamhuri kuhudhuria mbele ya Mahakama hii mnamo tarehe 16/07/2020 bila kukosa ili kuja kujibu madai hayo dhidi yenu. Endapo hamtahudhuria mbele ya mahakama siku hiyo shauri/mashauri hayo yatasikilizwa upande mmoja (Exparte Hearing) na kutolewa maamuzi. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Mahakama hii leo tarehe 01/07/2020.

115806202

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MONICA MAHENDA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T. 712 CZA,** AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2014 MAENEO YA SHABULUBA WILAYA YA SHINYANGA. KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA MONICA MAHENDA TILULI KWA SIMU NAMBA **0693921986.** **RB NAMBA SHY/RB/2020.**

115805602

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LYU FAN L** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 311 DNM** aina ya Toyota Kluger. Chassis namba **ACU250004742.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi
**MBE/MBE/RB/516083/2020.**

115805001

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATES'S COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**

**APPL. OBJ. PROC. No. 06 OF 2020**

**(Arising from District Court of Bukoba at Bukoba Civil case No. 42 of 2002)**

**GRACE PASTORY .......................................OBJECTOR**

**VERSUS**

**M/S KOLPING SOCIETY OF TANZANIA ..........1st RESPONDENT**
**STANLEY ISHUNGA .......................2nd RESPONDENT**
**DEOGRATIAS KATABARO..............3rd RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING**

**TO: STANLEY ISHUNGA**

**TAKE NOTICE** that the mentioned case has been set down for Hearing on the **17 th day of July, 2020 at 8:30 O'clock** in the forenoon, Before **Hon. J.P. KAPOKOLO - SRM.** your presence is therefore required on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this 3rd day of July, 2020

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

115804702

---


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA

# NMB yasaidia shule Tanga mil. 36/-

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya NMB imetoa msaada wenye thamani ya Sh.milioni 36 kwa shule saba za sekondari za jijini Tanga kwa ajili ya kusaidia kutatua changamoto za kielimu.

Akikabidhi msaada huo katika shule ya sekondari ya Pongwe, Ofisa Mkuu wa fedha wa benki hiyo, Benedicto Baragomwa, alisema kuwa msaada huo ni sehemu ya kurudisha fadhila kwa jamii.

Alisema kuwa kutokana na kutambua juhudi kubwa za maendeleo zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano, benki hiyo imeona ipo haja ya kuhakikisha inatoa sehemu ya faida yake katika kuchangia juhudi hizo.

"Changamoto katika sekta ya elimu ni miongoni mwa vipaumbele vyetu kama benki kwani tumekuwa tukishiriki kusaidia jamii na katika sekta ya afya," alisema Baragomwa.

Pia alisema kuwa katika kipindi cha miaka minne, benki hiyo imechangia zaidi ya Sh. bilioni 4 kwa ajili ya kusaidia jamii katika ununuzi wa vifaa tiba 330 kwa hospitali na vituo vya Afya zaidi ya madawati 31,150 pamoja na kompyuta 1,150 nchi nzima.

"Kwa mwaka huu NMB imetenga zaidi ya Sh.bilioni 1 kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya jamii ikiwamo kusaidia sekta ya afya na elimu"alisema Baragomwa.

Kwa upande wake Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema kuwa elimu bure imesaidia watoto wengi wa kike kupata fursa ya elimu tofauti na hapo awali.

Ummy alisema kuwa jitihada za serikali katika kuboresha mazingira ya kujifunzia ni katika kuhakikisha wanaongeza ufaulu kwa wanafunzi.

"Tunawashukuru NMB kwa kutuunga mkono katika jitihada za kumaliza changamoto za kielimu katika jiji la Tanga hususani katika upande wa uhaba wa vyumba vya madarasa pamoja na madawati," alisemaUmmy.

Benki hiyo ilitoa msaada wa madawati 250 pamoja na mabati 352 kwa shule za sekondari Kirare, Japan, Chongoleani, Nguvumali, Pongwe na Galanos.




Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (kushoto), akitoa maelezo kwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kulia), kabla ya kumkabidhi msaada wa madawati na mabati katika viwanja vya shule ya sekondari Pongwe, jijini Tanga jana. NMB imetoa madawati na viti 350 na mabati 352 kwa shule saba za jiji hilo. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Kortini kwa madai ya uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI wawili wa mkoani Arusha, Seuri Kisamu maarufu kama Mollel (34) na Losieku Mollel (35), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, wakikabiliwa na kesi mbili tofauti za uhujumu uchumi ikiwamo kukutwa na kilo 1,378.4 za bangi.

Katika kesi ya kwanza, Kisamu amesomewa shtaka lake mbele ya Hakimu Mkazi Gwantwa Mwankuga.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa Juni 30, mwaka huu, katika kijiji cha Englion, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, mshtakiwa alikutwa akisafirisha kilo 649.5 za bangi kinyume cha sheria.

Katika kesi ya pili, ilidaiwa mbele ya Hakimu Mwankuga kwamba siku ya kesi ya kwanza, mshtakiwa Losieku alikutwa akisafirisha bangi kilo 728.9 huku akijua ni kinyume cha Sheria.

Washitakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka kisheria kusikiliza kesi za uhujumu uchumi mpaka upelelezi utakapokamilika na kuhamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Rushwa, maarufu kama Mahakama ya Mafisadi.

Hakimu Mwankuga alisema kesi hiyo itatajwa Julai 22, mwaka huu, na washtakiwa wapelekwe mahabusu.

# Shirika lataka waathirika likizo ya corona kusaidiwa

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Ubadilishaji Wanawake limezitaka shule na wadau wengine wanaoshughulika na masuala ya kutetea haki za watoto nchini, kuja na mikakati maalum ya kusaidia baadhi ya watoto walioathiriwa na vitendo vya ukatili wakati wa likizo ya miezi mitatu ya Covid-19.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuhakikisha kunaanzishwa vyumba maalum shuleni kwa ajili ya kutolea huduma kwa watoto hao watakaothibitika kuathiriwa na uwapo wa janga la ugonjwa wa corona pamoja na aina nyingine za unyanyaji waliokumbana nao katika kipindi chote walichokuwa nyumbani.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Shirika la Mabadiliko na Kujenga Ushirikiano kwa wote(TIBA), Malcela Lungu, alisema baada ya shule kufunguliwa kuna haja ya kuwa na mikakati madhubuti ya kuwalinda watoto katika vipindi vya majanga kama hayo na pia wanapokuwa nyumbani na shuleni.

"Kuna watoto ambao walikabiliwa na changamoto mbalimbali za dhuluma kama vile ubakaji, kupigwa na vitendo vingine vya kikatili wakati wa likizo jambo ambalo linapaswa pia kuzingatiwa kwa kuangalia namna ya kuwasaidia pia kisaikolojia," alisema Lungu.

Kwa upande wake, Ofisa kutoka TIBA, Salim Mtepellah, alisema kuwa shirika limekuwa likitoa mafunzo ya kupambana na ukatili wa kijinsia na namna ya kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona tangu uingie nchini na kwamba kuna idadi kubwa ya wanawake wanaopitia wakati mgumu katika jamii zao ikiwamo vitendo hivyo vya ukatili.

## HABARI MICHEZO



# SIJAONA

## MCHEZAJI KAMA SILVA - GUARDIOLA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amedai kamwe hajawahi kuona mchezaji kama David Silva baada ya kiungo huyo kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati Manchester City wakiibuka na ushindi wa 5-0 dhidi ya Newcastle United.

Silva alitengeneza mabao ya Gabriel Jesus na Raheem Sterling na alifunga kwa shuti kali la adhabu ndogo wakati City walipafanya kazi ya kuvutia dhidi ya vijana hao wa Steve Bruce, Jumatano kwenye Ligi Kuu ya England.

Kiungo huyo raia wa Hispania sasa amefikisha pasi za mwisho 121 pale City na amefikisha 10 katika mashindano yote katika misimu yake 10 na klabu hiyo.

Silva atakuwa na mechi mbili zaidi za ligi za nyumbani kabla ya kuondoka City mwishoni mwa msimu huu, huku kuagwa kwake hakutahudhuriwa na mashabiki kutokana na kutoruhusiwa kuingia uwanjani kutokana na mlipuko wa virusi ya corona.

Na kocha Guardiola bado ana matarajio ya Silva kuagwa kama ilivyopangwa, na anaamini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 ni tofauti na mchezaji mwingine yoyote.

"Kwa kiwango alichofikia nafikiri yeye ni bora kwa msimu huu," alisema Guardiola akiiambia BT Sport.

"Anacheza kwa kiwango cha kuvutia, kwa uhakika kabisa yeye ni mzuri. Ndio, mashabiki hawatakuwa pale, lakini atakuja kuagwa mbele ya mashabiki."

## KLOPP: SALAH ANATAKA KIATU CHA DHAHABU

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah anahamasa ya kushinda tena kiatu cha dhahabu kwenye Ligi Kuu ya England, kwa mujibu wa kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp.

Salah alifunga mabao mawili wakati Liverpool ikiichapa Brighton and Hove Albion mabao 3-1 Jumatano kwenye mchezo wa Ligi Kuu, na kuwafanya mabingwa hao wa EPL kufikisha pointi 92 msimu huu.

Fowadi huyo alishinda kiatu cha dhahabu misimu miwili iliyopita, huku msimu uliopita alishinda kwa pamoja na Sadio Mane na Pierre-Emerick Aubameyang.

Klopp alisema tuzo hiyo imemhamasisha tena nyota huyo wa kimataifa wa Misri, ambaye ana mabao 19 ya ligi msimu huu, akipitwa na nyota wa Leicester City, Jamie Vardy mwenye mabao 22 na fowadi wa Arsenal, Aubameyang mwenye mabao 20.

"Yeye ni mshambuliaji, namna gani asiwe na hamasa? Hili liko wazi kabisa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Katika miaka miwili iliyopita alishinda kiatu cha dhahabu, mwaka jana alishinda kwa pamoja na Sadio na Auba. Hilo mara zote ni muhimu, ni muhimu kwa Sadio na wachezaji wote.

"Mwisho wa siku unaweza tu kufunga mabao wakati kiwango chako kipo juu na anauwezo wa kufanya hivyo."

Salah amekuwa mchezaji wa nne wa Liverpool kuhusika katika mabao 100 kwenye Ligi Kuu, akiwa na mabao 73 na pasi za mwisho 27 kwenye mechi 104.

Ana mabao 94 kwa Liverpool, pamoja na Mane (79) na Roberto Firmino (77), watatu hao wamefikisha jumla ya 250 kwa klabu hiyo katika mashindano yote.




## SOLSKJAER ANATUMAINI POGBA ATASAINI MKATABA MPYA

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer ana matumaini kiungo wake nyota, Paul Pogba atasaini mkataba mpya pale Old Trafford.

Majaliwa ya Pogba yametawala vichwa vya habari msimu huu wote, huku mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa akiripotiwa kutokuwa na furaha pale Manchester huku akihusishwa na klabu yake ya zamani Juventus na Real Madrid.


Lakini Pogba, ambaye amekuwa na majeruhi ya mara kwa mara msimu huu, amekuwa kwenye kiwango kizuri tangu aliporudi dimbani baada ya kuumia kifundo cha mguu mwezi uliopita, akionekana kuwa na upatina mzuri na Bruno Fernandes kwenye safu ya kiungo.

Mkataba wa Pogba na miamba hao wa Ligi Kuu unamalizika mwaka 2021, huku kukiwa na kifungu cha kuongeza mwaka mmoja, na Solskjaer anaangalia uwezekano wa kuanza mazungumzo mapya na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 baada ya Nemanja Matic na Scott McTominay kusaini.

"Siwezi kuzungumza chochote kuhusu majadiliano kati ya mchezaji na klabu, tunataka kuwabakiza wachezaji bora klabuni," alisema Solskjaer kabla ya mchezo wa jana Alhamisi dhidi ya Aston Villa.

**"Tunataka kujenga kikosi kwa ajili ya baadaye na Scott na Nemanja walikuwa kwenye hali kama hiyo, lakini hatua to fauti katika maisha yao ya soka. Mmoja ndio anaanza na mwingine ana uzoefu wa kuto sha."**

## HABARI MICHEZO



# DORTMUND
## KUTAFUTA MRITHI WA SANCHO

**DORTMUND, Ujerumani**

MKURUGENZI wa soka wa Borussia Dortmund, Michael Zorc, amesema kikosi hicho cha Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kinawania kuimarisha safu ya ulinzi kama Jadon Sancho anayewindwa na Manchester United ataondoka.

Sancho amekuwa akihusishwa sana na mpango wa kujiunga na miamba hao wa Ligi Kuu ya England, huku klabu nyingine kama Liverpool, Chelsea na Real Madrid pia zinatajwa kumuwinda.

Dortmund imeripotiwa kwamba inataka euro milioni 120 kwa ajili ya nyota huyo wa kimataifa wa England, ambaye aliwasili pale kutoka Manchester City mwaka 2017.

Alipoulizwa kuhusu uwezekano wa Sancho kuondoka, Zorc aliliambia gazeti la Kicker: "Kama Jadon ataondoka, tutafanya kitu fulani kwenye safu ya ushambuliaji.


"Kuna mchezaji mmoja au wawili ambao tunawawania kwa sasa."

Sancho alifunga mabao 17 na kutoa pasi za mwisho 16 wakati Dortmund ikimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Bundesliga nyuma ya mabingwa Bayern Munich msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 amefunga mabao 20 katika mashindano yote msimu huu 2019-20.

Dortmund, imetajwa kuwania kumsajili nyota wa Birmingham City, Jude Bellingham ambaye anawaniwa na United.

## ERIC DIER AFUNGIWA MECHI NNE



**LONDON, England**

ERIC Dier amefungiwa mechi nne na kutozwa faini ya pauni 40,000 baada ya kuhusika kwenye ugomvi na shabiki wakati Tottenham ikipoteza kwenye mchezo wa FA dhidi ya Norwich City, Machi mwaka huu.

Kiungo huyo wa England alipanda jukwaani kwa mashabiki baada ya Spurs kupoteza kwa mikwaju ya penalti kwenye uwanja wa Tottenham Hotspur.

Walinzi wa Stewards waliingilia kati kumwondoa Dier kutoka kwa shabiki, huku kocha Jose Mourinho baada ya tukio hilo alisema mchezaji huyo alichukizwa na matusi dhidi ya mdogo wake.

Dier alishtakiwa na chama cha soka cha England, FA, Aprili mwaka huu.

Alikanusha madai hayo, lakini mamlaka ya tume huru ilimkuta na hatia na FA ilithibitisha Jumatano kumpa adhabu hiyo.

"Eric Dier amefungiwa mechi nne kuanzia sasa, na faini ya pauni 40,000 na ameonywa kuhusu tabia yake kwa siku za usoni kwa kuvunja kanuni ya FA ya E3," ilisomeka taarifa ya FA.



## HENDERSON AMPASUA KICHWA KLOPP

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp hana uhakika kiwango cha majeruhi ya Jordan Henderson alivyoumia wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Brighton na Hove Albion.

Nahodha wa wekundu hao aliifungia timu yake bao la pili kwenye mchezo huo wa Jumatano, akimaliza mpira uliotemwa na kipa Mat Ryan sekunde 127 baada ya Mohamed Salah kuwaweka mbele mabingwa hao.

Hata hivyo, Henderson alitolewa dakika ya 80 akionekana kuumia goti na Liverpool watatakiwa kusubiri kujua atapona kwa muda gani.

"Sijui (ameumia kwa kiasi gani), kwa kweli sijui kabisa," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Sikuweza kuona kilichotokea uwanjani, lakini najua kwamba ameumia na sijajua atapona baada ya muda gani. Hivyo siwezi kusema mengi."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SUAREZ: BARCELONA IWE TAYARI KWA REAL MADRID

●●●Asema wana nafasi kama wapinzani wao watapoteza pointi na kitu kinachotakiwa ni...

**BARCELONA, Hispania**

LUIS Suarez amesema Barcelona lazima iwe tayari kama vinara wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Real Madrid watapoteza pointi kwenye mbio za kuwania ubingwa huo zinazoelekea mwishoni.

Bingwa mtetezi Barca walirudisha matumaini kwenye mbio hizo baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja, Espanyol, Jumatano.

Suarez alifunga bao hilo pekee kwenye mchezo huo katika dakika ya 56 na kuishusha daraja Espanyol, huku Barca wakipitwa pointi moja na Madrid.

Madrid wanaweza kuendelea kuongoza msimamo kwa pointi nne kama wataifunga Deportivo Alaves kwenye mchezo wa leo Ijumaa, huku Barca wakiwa wamebakiwa na mechi tatu pekee, na nyota Suarez amesisitiza miamba hao wa Katalunya wanatakiwa kuwa tayari kwa lolote.

**"Kitu tunachotakiwa ni kushinda mechi zetu tatu zinazofuata," alisema Suarez, ambaye alijivuta hadi nafasi ya tatu katika orodha ya wafungaji wa wakati wote wa Barca na kuongeza; "Chochote Madrid watakachofanya ni juu yao.**

"Kama watapoteza pointi litakuwa jambo zuri, tunatakiwa kufikiria kuhusu kuwa pale kama watafanya hivyo."

Barca hawakuwa kwenye kiwango chao bora kwenye mchezo huo uliopigwa katika dimba la Camp Nou, ambapo Ansu Fati aliyetokea benchi alitolewa kwa kadi nyekundu mwanzoni mwa kipindi cha pili, huku pia Espanyol walimpoteza Pol Lozano ambaye nae alilimwa kadi nyekundu.

Lakini Barca waliendelea kutofungwa kwenye mchezo wake wa tisa mfululizo.

Suarez aliongeza: "Tulijua itakuwa ngumu. Tulijua hali yao. Tunatakiwa kuhakikisha kwamba tunakuwa kwenye kiwango bora Jumapili na bado tunatakiwa kuangalia matokeo yake.

"Jambo la muhimu ni kushinda na kupata pointi zote tatu katika kila mchezo uliopo mbele yetu.

"Nafikiri kama nisingefunga au Barcelona wasingetengeneza nafasi, lingekuwa jambo gumu zaidi kwetu, tulijiimarisha sana."

## KWA UFUPI

**NORWICH YATAKA MIL. 50 KWA BEN**

NORWICH City inataka pauni milioni 50 kwa ajili ya mlinzi wake, Ben Godfrey mwenye umri wa miaka 22, huku klabu za Bundesliga, Borussia Dortmund na RB Leipzig ni miongoni mwa zinazomwania mchezaji huyo wa timu ya taifa ya England chini ya umri wa miaka 21. ***(Sky Sports)***

**HAVERT KUOMBA KUONDOKA BAYERN**

KIUNGO Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21, yupo tayari kutuma maombi ya uhamisho pale Bayer Leverkusen baada ya kuwaambia Chelsea anataka kujiunga nao kipindi cha majira ya joto. ***(Star)***

**CHELSEA MATUMAINI KIBAO KWA KAI**

CHELSEA ina matumaini Kai Havertz anataka kuungana na fowadi Timo Werner mwenye umri wa miaka 24, pamoja na Mjerumani mwenzake, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 27 pale Stamford Bridge. ***(Telegraph)***

**WAKALA WA BRUYNE AKANUSHA**

WAKALA wa Kevin de Bruyne amekanusha taarifa kwamba kiungo huyo mwenye umri wa miaka 29 raia wa Ubelgiji anapanga kuondoka Manchester City na kujiunga na Real Madrid au Paris St-Germain. ***(Sporza, via Star)***

**AJAX, SPURS MBIO KWA PIERRE-EMILE**

AJAX imeungana na Tottenham Hotspur katika mbio za kuwania kumsajili kiungo wa Southampton na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 24, huku Everton pia ikionyesha nia ya kumtaka. ***(Telegraph)***

**ANCELOTTI AHAKIKISHIWA EVERTON**

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti amesema "amehakikishiwa na bodi" kwamba klabu "itaimarisha" kikosi chake kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Guardian)***

**WAKALA ATIA NENO KWA GREALISH**

WAKALA wa kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 hajafikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na Manchester United, huku klabu yake ikimtaja kuwa na thamani ya pauni milioni 80. ***(Metro)***

**OZIL NI MAREKANI AU UTURUKI**

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 31, anataka kuhamia Uturuki au Marekani, lakini raia huyo wa Ujerumani ataondoka tu kwa washikabundi hao kama mkataba wake utamalizika. ***(Sun)***

**ARSENAL YAJITOSA KWA SARR**

ARSENAL imetoa ofa ya kutaka kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Malang Sarr baada ya kuondoka Nice, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka RB Leipzig kwenye mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Marca, via Express)***

**SPURS YAMTAKA KURT**

KLABU ya Tottenham Hotspur inawania kumsajili mlinzi wa kati wa Ufaransa, Kurt Zouma kutoka Chelsea, ingawa nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 pia anawindwa na Everton. ***(Express)***

**JUVENTUS YAIPA OFA CHELSEA**

JUVENTUS imeipa ofa Chelsea kuchukua wachezaji wawili, akiwamo kiungo wa kimataifa wa Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 29, kwa ajili ya kubadilishana na kiungo wa Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 28. ***(Express via Tuttosport)***

HABARI MICHEZO

# MATOLA AFUNGUKA SIMBA ILIVYOKAMIWA MSIMU HUU

**Na Somoe Ng'itu, RUANGWA**

KOCHA Msaidizi wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Selemani Matola, amesema timu yao haikuwa na kazi rahisi katika safari yao ya kutetea ubingwa wa ligi hiyo inayotarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi huu.

Simba ilifanikiwa kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa tatu mfululizo tangu Juni 28, mwaka huu, ilipotoka sare ya bila kufungana na Maafande wa Tanzania Prisons jijini, Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matola alisema mechi zote walizocheza msimu huu zilikuwa ngumu kwa sababu walikuwa wanapambana na klabu zinazoutamani ubingwa walioushikilia.

Matola alisema kila timu iliamini ikiwafunga Simba, itakuwa tumejiweka katika nafasi nzuri ya kuwania taji hilo na hivyo mechi zao zote zilikuwa na ushindani wa kiwango cha juu.

Nahodha huyo wa zamani wa Simba, alisema anawapongeza wachezaji wao kwa kupambana katika kila mechi waliyocheza na kutokana tamaa hata pale walipopoteza mchezo au walipolazimishwa sare.

"Safari yetu ilikuwa ngumu sana, ilikuwa tunapambana na timu zote 19, kila timu ilijipanga zaidi kutufunga ili kujiimarisha katika kutimiza malengo yake, kwa hiyo kila mchezo kwetu ilikuwa ni sawa na fainali, walijua wanacheza na bingwa mtetezi, watufunge ili wajirahisishie mipango yao," alisema Matola.

Aliongeza kuwa pongezi nyingine ziende kwa mashabiki, viongozi na wanachama wa Wekundu wa Msimbazi kwa kushirikiana pamoja kuanzia mwanzo wa msimu hadi mwisho wa safari yao ya kufunga msimu.

"Tuliianza safari pamoja, hawakutuacha, ninaamini tutaendelea pamoja katika kumalizia msimu kwenye mashindano ya Kombe la FA yaliyoko mbele yetu," alisema kiungo huyo wa zamani wa Simba na Super Sport ya Afrika Kusini.

Mabingwa hao wamebakiza mechi nne ambazo ni dhidi ya Mbao, Alliance, Coastal Union na Polisi Tanzania itakayochezwa kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika mjini Moshi, Kilimanjaro.

Kikosi cha Simba kilirejea jijini Dar es Salaam jana asubuhi na jioni ilitarajiwa kuanza maandalizi ya kuwakabili watani zao, Yanga katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la FA itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa.



Msanii wa vichekesho, Idris Sultan (kushoto), akiwa na mwanasheria wake wakitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi inayomkabili ya matumizi mabaya ya mitandano ya kijamii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ushindani zaidi watarajiwa Bara

**Na Somoe Ng'itu, RUANGWA**

WAKATI Bodi ya Ligi Kuu Nchini (TPLB), ikisema msimu ujao unatarajiwa kuwa na ushindani zaidi, bado inafurahi kuona klabu zinapambana kuhakikisha zinasalia kwenye ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa bodi hiyo, Almasi Kasongo, aliliambia Nipashe jana licha ya bingwa kuwa ameshapatikana, bado klabu zinachuana kuwania nafasi ya pili ambayo wanaiita ya heshima.

Kasongo alisema pia klabu nyingine zinapambana zaidi kuhakikisha zinajiepusha na hatari ya kushuka daraja na hakuna ambaye amekata tamaa kwenye vita hiyo.

Alisema kila mechi imekuwa na ushindani na kila timu inaposhuka uwanjani inapambana kupata matokeo mazuri, ili kuhakikisha inafikia malengo yake.

"Sisi kama wasimamizi wa ligi tunasema tumefanikiwa, ushindani umeongezeka, huku tukiwa tayari tumeshampata bingwa, lakini mechi zilizobakia kila timu inacheza kwa malengo yake, kuna wanaowania nafasi ya pili ambao ni Azam, Yanga, Namungo na Coastal Union, ila pia kuna timu sita zinazojikwamua kujiondoa kwenye mechi za mtoano," Kasongo alisema.

Aliongeza bodi inaamini msimu ujao ligi hiyo itakuwa bora zaidi kwa sababu timu zitakazoshiriki zitapungua na klabu zitataka kukamilisha 'hesabu za ubingwa' mapema badala ya kusubiri mechi za lala salama.

Kiongozi huyo alizipongeza timu zote zinazoshiriki ligi hiyo ambayo ni moja ya ligi maarufu kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao itashirikisha klabu 16, na kwa maana hiyo, timu nne zitakazoburuza mkia msimu huu itashuka daraja moja kwa moja wakati nyingine mbili zitapambana katika michezo ya mtoano ili kusaka tiketi ya kubakia kwenye ligi hiyo.

## KVZ kuionyesha kazi leo JKU

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa timu ya KVZ, Sheha Khamis amesema mchezo wake wa leo, dhidi ya JKU utakuwa mgumu kwa sababu timu anayokutana nao inawania ubingwa, huku wao wanapigania kutoshuka daraja.

Akizungumza na Nipashe, Khamis alisema licha ya timu yake kujiandaa katika kuhakikisha michezo yake mitano iliyobaki anafanya vizuri, lakini bado kuna ushindani mkubwa kwa timu ambazo zinawania ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Alisema katika kipindi hiki cha kuelekea ukingoni mwa msimu, ligi inakuwa ngumu, kwa sababu bado haijulikani timu gani itatwaa ubingwa.

"Ligi ikielekea ukingoni mwa msimu, huku bingwa akiwa hajajulikana inakuwa ngumu sana, maana waliokuwa tatu bora wanahangaika kuutafuta ubingwa na timu zilizobaki hazina uhakika wa kubaki Ligi Kuu," alisema.

Aidha, alisema mchezo huo wa leo dhidi ya JKU utawakosa wachezaji wake wawili muhimu walioumia mazoezini ambao ni mlinzi wa kati, Mohamed Nassor na mshambuliaji, Mabaadi Maulid.

## Mwakinyo kumvaa Mkongo mwezi ujao

**Na Faustine Feliciane**

BONDIA Mtanzania Hassan Mwakinyo anatarajia kupanda ulingoni Agosti 14 mwaka huu kumenyana na bondia kutoka Congo, Tshibangu Kayembe.

Pambano hilo la aina yake la kuwania ubingwa wa WBF linatarajiwa kufanyika katika Ukumbi wa Mlimani City, ambapo mabondia hao watapambana raundi 12.

Akizungumzia pambano hilo Mwakinyo amesema yuko tayari kupanda ulingoni kwa sababu amejiandaa vya kutosha kuhakikisha anamaliza pambano hilo mapema.

Amesema, maandalizi mazuri ambayo ameyafanya na kuendelea kuyafanya yanazidi kumpa morali zaidi kuelekea pambano hilo ambalo hatokubali kuiangusha nchi.

"Tarehe 14 mwezi ujao natamani sana pambano lifike hata siku zikimbie tano tano, nimejiandaa na naendelea kujiandaa sina shaka wala hofu na bondia yeyote yule aje tu tukutane ulingoni," alisema.

Aidha, Mwakinyo alimwomba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania John Magufuli kuunga mkono jitihada za mabondia hapa nchini kama ambavyo amefanya mambo makubwa katika kuendeleza nchi na jina lake kuzidi kuwa kubwa.

Anasema Rais akisapoti mchezo huo hata wao mabondia itakuwa vyema kwao na itazidi kuwapa morali ya hali ya juu kuzidi kulitangaza Taifa.

"Naimani kubwa na Rais wetu pia nawaomba wadhamini nao wasiutupe mchezo wetu huu unapeperusha vyema bendera ya Tanzania kupitia sisi na hiyo Agosti 14 nitawahahakikishia Watanzania mimi ni nani."

Michezo
Ijumaa Julai 10, 2020
Nipashe

HABARI UK 22



Suarez: Barcelona iwe tayari kwa Real Madrid



Mshambuliaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, akishangilia baada ya kufunga bao dhidi ya Leicester City katika mchezo wa Ligi Kuu ya England baina ya timu hizo, juzi kwenye uwanja wa Emirates. Timu hizo zilitoka sare bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# SVEN ATENGA SAA 48 HATARI

Mbelgiji huyo aeleza wanataka kukamilisha hesabu za msimu huu kibabe, Manara atamba Jumapili hawachomoki...

**Na Somoe Ng'itu, RUANGWA**

BAADA ya kukabidhiwa kikombe cha ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema leo ndio anaanza kupanga mikakati ya ushindi kuelekea mchezo wao wa nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Yanga utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe mjini hapa, Sven, alisema hakutaka kuufikiria mchezo huo mapema kwa sababu anaifahamu vema Yanga hivyo, safari hii wasubiri kuona makali na hasira za kikosi chake.

Sven alisema hata walipokuwa wakiwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, baadhi ya wapinzani wao walikisema kikosi chake lakini mwisho wake wameshuhudia kombe likitua Msimbazi kwa msimu wa tatu mfululizo.

Mbelgiji huyo alisema mechi hiyo kwake ni rahisi kwa sababu amebakiza "hesabu" za kuwania taji hilo bila ya presha ya kuwaza tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa kama walivyo watani zao Yanga.

"Sikuwahi kuifikiria Yanga, wacha kwanza tufike Dar es Salaam, halafu ndio tuanze mikakati ya kuelekea mchezo huo wa nusu fainali, tutakuwa na siku mbili za mazoezi, zinatosha kuimarisha mipango yetu," alisema Sven.

Kocha huyo alisema atakuwa na uhuru wa kupanga kikosi chochote baada ya baadhi ya nyota wake kupumzika katika mchezo uliopita dhidi ya Namungo FC ambao ulimalizika kwa suluhu.

"Sitaki kuwaahidi mashabiki nini tutafanya, hii imebaki baina yangu na wachezaji, nitazungumza na kuwaambia wanachotakiwa kukifanya Jumapili, tusubiri," Mbelgiji huyo aliongeza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Setho Mbatha, alisema mechi hiyo itakuwa ngumu na wamejiandaa kukabiliana na ushindani kutoka kwa watani zao.

Mbatha alisema wanajua Yanga wataingia na presha ya kutaka ushindi kujihakikishia na safari ya kuchukua kombe hilo ili washiriki mashindano ya kimataifa, huku wao wakikataa kupoteza tena dhidi ya vigogo hao.

"Itakuwa na ushindani kutoka pande zote mbili, kila timu itaingia kuhakikisha malengo yake yanafanikiwa, kwetu tumejipanga kuhakikisha haturudii makosa, kupoteza tena mchezo wa 'dabi' haiwezekani, tunahitaji kufanya nguvu ya ziada kama mabingwa," Mbatha alisema.

Aliongeza anafurahi kuona msimu wake wa kwanza wameshinda taji la Ligi Kuu Tanzania Bara na anatarajia kukamilisha furaha ndani ya klabu hiyo kwa kulipa kisasi cha kufunga Yanga na kuiondoa kwenye kampeni ya kuwania kombe hilo la tatu msimu huu.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, Haji Manara, aliendelea kutamba timu hiyo imeshachukua makombe matatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa yamebaki saba katika mkakati wao wa kushinda mara 10 mfululizo.

Manara aliwataka watani zao Yanga pamoja na timu nyingine wasiweze mawazo ya kushinda taji hilo mpaka kuanzia mwaka 2027 ambapo wao wanaweza kuliachia.

"Kesho (jana) tutakuwa na sherehe za ubingwa, tutalikabidhi kombe letu pale klabuni, halafu tutaanza mikakati ya kuwamaliza Yanga, watatueleza walichomokaje siku ile, watatoa jibu Jumapili," Manara alitamba.

Mbali na mchezo huo, nusu fainali nyingine itakuwa kati ya Namungo FC dhidi ya timu ya Daraja la Pili, Sahare All Stars ya jijini, Tanga.

## EYMAEL AWATIA MZUKA YANGA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, amesema anajua kikosi chake hakina namna yoyote ya kuweza kushiriki michuano ya Kimataifa endapo hawatatwaa ubingwa wa FA, na sasa ameweka bayana kwamba lazima washinde mchezo wao dhidi ya Simba.

Yanga wanakutana na Simba Jumapili kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe, Eymael alisema matokeo ya mechi yao ya juzi dhidi ya Kagera Sugar ya bao 1-0 yalikuwa ni maandalizi kwa ajili ya mchezo wao huo dhidi ya Simba na ni lazima washinde.

Alisema anaamini mchezo huo utakuwa mgumu kwa dakika zote 90, lakini amewaandaa wachezaji wake kumaliza kazi mapema.

"Hii mechi itakuwa ngumu sana, kwa sababu Simba wanataka kulipa kisasi kwani tuliwafunga mchezo uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini wote tunataka kuingia fainali na kutwaa ubingwa huu," alisema.

"Sisi mchezo huu una umuhimu mkubwa sana kwetu, kwani inaweza ikawa njia ya kushiriki michuano ya kimataifa, na tumejiandaa tunamaliza kazi mapema," alijigamba Eymael.

Alisema kuna mambo mengine hawezi kuweka wazi kikubwa wanaendelea na maandalizi kuhakikisha kikosi chake kinakuwa kwenye hali nzuri.

Kocha huyo raia wa Ubelgiji aliongeza kusema, hawataki kupoteza mchezo huo sababu ndio nafasi pekee ya wao kuweza kufuzu kushiriki michuano ya kimataifa msimu huu.

Akizungumzia wachezaji wake, alisema kiungo wake, Haruna Niyonzima anaendelea vizuri, lakini ni mapema kuweka wazi kuwa atacheza kwenye mchezo huo, kwa sababu anaangalia kwanza ufiti wake baada ya kuumia katika mchezo na Biashara.

Katika mchezo huo, Yanga watakuwa na kazi moja tu ya kuhakikisha wanashinda ili kupata nafasi hiyo ya kushiriki michuano ya kimataifa.

Yanga watamtegemea zaidi kiungo wao, Bernard Morrison, ambaye ndiye aliyewalaza na viatu wekundu hao wa Msimbazi Machi 8 mwaka huu, akifunga bao pekee kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara mzunguko wa pili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >